# Nipashe

Jumatatu Mei 6, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579910

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## NSSF yaanza malipo ya wanachama kwa mtandao

UKURASA 3




UKURASA 13

# Barabara ya mwisho Dk. Reginald Mengi

• **Viongozi**, wananchi wamiminika nyumbani kumlilia... *Endelea ukurasa 2*

### NJIA UTAKAPOPITA MWILI




## 91,442 kufanya mitihani kidato 6

UKURASA 2



Baadhi ya watu wenye ulemavu wakilia wakati wakiwasili nyumbani kwa marehemu Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk Reginald Mengi, Kinondoni jijini Dar es Salaam jana. Mwili wa Dk Mengi unatarajiwa kuwasili nchini leo kutoka Dubai. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

## Hiace ilivyoua watu 10, kujeruhi 12 Kigoma

UKURASA 3


**MICHEZO** YANGA, LIPULI FC HAPATOSHI IRINGA UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Barabara ya mwisho ya Dk. Mengi

Na Mary Geofrey

SERIKALI imesema ulinzi umeimarishwa katika maeneo ambako mwili wa aliyekuwa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, utapita leo baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) ukitokea Dubai, Falme ya Kiarabu.

Aidha, amewataka wananchi wajitokeze kwa wingi kuanzia uwanja wa ndege kuazia saa 8:00 mchana na katika maeneo yote utakapopita mwili huo kwa ajili ya kutoa heshima za mwisho kwa Dk. Mengi, ambaye alijitoa kwa ajili ya maisha ya watu wanyonge na wasiyojiweza.

**MAENEO UTAKAKOPITA**

Hayo yalisema jana na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, alipozungumza na Nipashe, na kutaja maeneo ambako mwili huo utapita ni barabara ya Uwanja wa Ndege, Vingunguti, Buguruni, Karume (Ilala), Kigogo, Magomeni (Kanisa Katoliki), Tandale, Sinza, Kijiweni, Bamaga, ITV, Mwenge kuelekea Lugalo.

"Mkoa wa Dar es Salaam kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama vya mkoa likiwamo Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, tumejipanga kuimarisha usalama katika maeneo yote ambako mwili wa mpendwa wetu, Dk. Mengi utapita," alisema Makonda.

Alisema pia wamejipanga kuimarisha ulinzi na usalama kwa siku tatu ambazo mwili huo utakuwa katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Alifafanua kuwa siku ya kwanza ni leo ambayo mwili utawasili, siku

INAENDELEA UK. 8



Mtendaji Mkuu Azam Media, Tido Mhando, akimzungumzia Dk. Mengi akiwa nyumbani kwa marehemu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA SELEMANI MPOCHI**

## 91,442 kidato cha 6 kufanya mitihani leo

Na Romana Mallya

JUMLA ya watahiniwa 91,442 wamesajiliwa kufanya mitihani ya Kidato cha Sita inayotarajia kuanza leo nchini huku Baraza la Mitihani (Necta), likitoa onyo kali kwa wadanganyifu.

Katibu Mtendaji wa Necta, Dk. Charles Msonde, aliyesema hayo jana jijini Dar es Salaam na kubainisha kati ya watahiniwa wote waliosajiliwa kufanya mtihani huo, watahiniwa wa shule ni 80,305 na wa kujitegemea ni 11,117.

"Baraza halitasita kumchukulia hatua mtu yeyote atakayebainika kujihusisha au kusababisha udanganyifu wa mitihani hii inayoanza kesho (leo)," alisema.

Dk. Msonde alisema kati ya watahiniwa wa shule, wasichana ni 34,081 sawa na asilimia 42.44 na wavulana ni 46,224 sawa na asilimia 57.56.

"Watanihiwa wenye mahitaji maalum wapo 102 kati yao 67 ni wenye uoni hafifu, 16 ni wasioona, 18 wenye ulemavu wa kusikia na mmoja mwenye ulemavu wa akili," alisema.

Alisema ikilinganishwa na mwaka jana, idadi ya watahiniwa waliosajiliwa kufanya mtihani huo walikuwa ni 77,222 hivyo kuna ongezeko la jumla ya watahiniwa 3,083 sawa na asilimia nne kwa mwaka huu.

INAENDELEA UK. 8

# ...Wengi waendelea kumlilia

Na Romana Mallya

MAKUNDI mbalimbali ya jamii wakiwamo viongozi wa serikali, sekta binafsi na taasisi za fedha wameendelea kumlilia Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, huku wakisema alikuwa na mchango mkubwa kwao wa kimawazo na kifedha.

**ABDULMAJID NSEKELA**

Wakizungumza kwa nyakati tofauti baada ya kufika nyumbani kwa marehemu Kinondoni jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema kwenye benki hiyo Dk. Mengi alikuwa mteja mkubwa.

"Yapo mengi ya kujifunza kutoka kwake, alikuwa mzalendo wa kweli, alipenda kuona Watanzania wengi wanaendelea kuijenga nchi yake, alikuwa mteja wetu mkubwa amekuza wafanyabiashara wengi," alisema.

**TIDO MHANDO**

Mtendaji Mkuu, Azam Media, Tido Mhando, alisema pamoja na kwamba Dk. Mengi amefariki na umri wa miaka 77, lakini alikuwa na mawazo ya ujana zaidi kuliko kundi hilo.

"Alipoamua kuanzisha IPP Media miaka ya katikati ya 90, watu wengi walifikiri kwamba anaingia mahali ambako hakuna tija, lakini Dk. Mengi aliwapa chachu inayostahili vijana na akahakikisha anawakusanya wale wenye uwezo ili kuhakikisha tasnia ya habari inakua," alisema.

Akizungumzia kuhusu kitabu chake cha I Can, I Must, I Will, Mhando alisema wapo walijiuliza kwa nini kaamua kukiandika.

"Amefanya jambo la ajabu ambalo kwa kawaida Watanzania wengi hatufanyi, mwaka jana alizindua kitabu cha maisha yake ambayo ameyaandika kwa uwazi, wengine wakafikiri kwa nini kaandika haya? kwa nini kajiachia hivi? Mungu alishampa nuru ya kumwambia kipindi chake kinakaribia cha kuondoka duniani," alisema.

**KIONDO MSHANA**

Mkurugenzi Mtendaji mstaafu wa The Guardian Ltd, Kiondo Mshana, alisema Dk. Mengi ndiye aliyemkuza na kumpandisha hadi kushika nafasi ya juu kwenye kampuni yake.

"Nilikuwa Sub Editor (Mhariri Msanifu) nikapanda hadi kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa The Guardian, nilikwenda kijana hadi nikawa mzee," alisema.

Mshana alibainisha mambo mawili aliyojifunza kutoka kwa Dk. Mengi kuwa: "Nilijifunza huwezi kufanya kazi maisha yako yote, lazima ubadilike ufanye usajiriamali, limenisaidia sana, nilikuwa ninafanya kazi kwake, lakini niliangalia nikitoka nitakuwa nani?"

Pia alisema alimsaidia yeye na wenzake waliokuwa pamoja wakaanzisha chuo cha uandishi wa habari Times School of Journalism (TSJ) ambacho Dk. Mengi alifika na alitoa nafasi kwa wahitimu kufanya kazi kwenye vyombo vyake vya habari.

**ERICK SHIGONGO**

Mkurugenzi wa Kampuni ya Global Publishers, Erick Shigongo, alibainisha kuwa mwaka 1995 akiwa kijijini alitaka kuwa kama Dk. Mengi na mwaka 1998 alipokuja Dar es Salaam na kumtafuta bila kumpata akatimiza ndoto yake.

INAENDELEA UK.8


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
Tarehe 17/04/2019.

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMATATU** tarehe 06-05-2019 kampuni ya **S.S.F CO. LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **KAGERA,** gari hilo lenye namba za usajili:

   **T 785 CAD / T 298 BXS.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

   Urefu - mita 21.80
   Upana - mita 3.20
   Kimo - mita 5.20

3. Njia itakayotumika: **DAR ES SALAAM hadi KAGERA** kupitia **MWENDAKULIMA.**

   Gari itasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi** mpaka saa 12.00 jioni)

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

21521802

## HABARI KITAIFA



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma , Zuber White, akizungumza kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika Shule ya Msingi Karume, wilayani hapo juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Hiace ilivyoua 10, kujeruhi 12

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

Watu 10 wamefariki dunia na wengine 12 kujeruhiwa, baada ya gari walilokuwa wakisafiria kupasuka taili na kupinduka katika Kijiji cha Murela Wilaya ya Uvinza mkoani Kigoma.

Kamanda wa Polisi mkoa wa Kigoma, Martin Otieno, alisema tukio hilo lilitokea Mei Ijumaa majira ya saa 12 jioni katika kijiji hicho.

Otieno alisema chanzo cha ajali ni taili la nyuma kupasuka na dereva, Rajabu John, ambaye alikuwa anaendesha gari hiyo aina ya Toyota Hiace yenye namba za usajili T 247 BNG ambayo ilikuwa ikitokea Uvinza kuelekea Kigoma Mjini.

Kwa mujibu wa kamanda huyo, ilipofika katika Kijiji Murela ilipasuka taili na kupinduka na kusababisha vifo vya watu saba na majeruhi 12 katika eneo la tukio kwa sababu gari hilo lilikuwa ikifukuzana na gari nyingine.

Alisema dereva anashikiliwa na Polisi akiwa anapatiwa matibabu katika Hospitali ya Mkoa ya Maweni na baada ya matibabu, upelelezi ukikamilika atafikishwa mahakamani.

Kwa upande wake, nesi msimamizi wa hospitali hiyo, Ernest Joseph, alisema Mei 3, mwaka huu majira ya saa 12 jioni Hospitali ya Mkoa Maweni ilipokea majeruhi na maiti wa ajali hiyo.

INAENDELEA UK.8

# NSSF yaanza malipo ya wanachama kwa mtandao

**Na Salome Kitomari**

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), umeanza utaratibu wa kushughulikia madai mbalimbali ya wanachama kwa njia ya mtandao, ili kuondokana na usumbufu wa kwenda kwenye ofisi za mfuko.

Akizungumza na Nipashe katika mahojiano maalum hivi karibuni, Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Willium Erio, alisema utaratibu huo utajumuisha malipo kwa njia ya mtandao na kuachana na karatasi.

Alisema kwa kuanzia mfumo huo umekamilika kwenye makao makuu ya mfuko, ukafuatiwa na Kinondoni na baadaye watakwenda Ubungo na kusambaa nchi nzima.

"Tulianza na waajiri kuwa na namba maalum ya kulipia michango ya wanachama wetu kwa mfumo wa kielektroni wa malipo serikalini (GePG), kwa sasa hakuna mwajiri anayeruhusiwa kulipa bila namba maalum," alisema.

Alisema kila malipo yapo mtandaoni (online) na kwamba wanachana na utaratibu wa malipo dirishani kwa mwanachama kwenda kupokea hundi, bali moja kwa moja kwenda benki.

Erio alisema kwa sasa wamefikia hatua mstaafu akifungua madai analipwa moja kwa moja kwenye akaunti yake na hakuna utaratibu wa kwenda kwenye ofisi za mfuko.

"Tunafanya hivi ili kuondokana na mazingira ya rushwa, hakutakuwa na makaratasi au mfanyakazi wa mfuko kuonana na mwanachama hasa kwenye suala la malipo, ile njoo kesho nayo itapungua kwa kuwa kila kitu kitafanyika kidigitali," alisema.

Alisema ni matamanio ya NSSF kuwa mwanachama anaweza kutumia simu yake ya kiganjani kupata taarifa zake ikiwamo kuangalia salio badala ya kwenda ofisi za mfuko.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, kumekuwa na kusita kwa watumishi wengi kupokea mfumo huo, na kwamba hatua kwa hatua watawaelewa na utasambaa nchi nzima.

# Ajeruhiwa na simba kibandani kwa mamalishe

**Na Said Hamdani,** LINDI

KIZITO Mathey Mgogo (59), mkazi wa Kata ya Rutamba, Halmashauri ya Wilaya na Mkoa wa Lindi, amelazwa Hospitali ya Mkoa huo ya Sokoine, akiugulia majeraha aliyoyapata baada ya kushambuliwa na simba.

Alikumbwa na mkasa huo nyakati za usiku alipokuwa amejilaza katika kibanda cha mama lishe.

Mdogo wake, Michael Mathei, ndiye aliyebainisha tukio hilo alipokuwa akizungumza na mwandishi wetu aliyetembekea hispitali hiyo.

Michael alisema kaka yake ambaye ana tatizo la akili, alipatwa na mkasa huo usiku akiwa amejilaza kwenye kibanda kinachotumiwa na wajasiriamali wadogo (mamalishe) kuuza chakula.

Amesema siku hiyo Kizito akiwa anarejea nyumbani kutoka katika shughuli zake alipofika eneo la Namatili kilichopo kibanda hicho, kilichojengwa kwa kuzungushiwa fito maeneo ya pembeni bila kugandikwa kwa udogo, aliingia ndani na kujilaza.

"Hivyo alipoona ni usiku na mle ndani kuna moto, aliamua kuingia na kulala," alisema Michael.

Michael alisema wakati kaka yake akiwa kwenye usingizi simba wawili waliingia

INAENDELEA UK.8




# WFP, TADB kuwapa neema zaidi wakulima

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), wameahidi kushirkiana zaidi na kuongeza msukumo katika kuwasaidia wakulima nchini.

Taarifa ya pamoja iliyotolewa na taasisi hizo jijini Dar es Salaam Jana, ikisema kwamba kwenye kikao chao cha hivi karibuni, walijadiliana na kukubaliana maeneo mapya ya kushirikiana ili kuendeleza sekta yakilimo nchini.

"Ubunifu ni muhimu sana katika kukifanya kilimo kuwa cha kisasa nchini, TADB na WFP wanafanya kazi ya kuhakikisha kwamba nyanja hii inapewa kipaumbele kwenye kilimo hapa nchini kwa namna mbalimbali," taarifa hiyo ilisema.

Taarifa inasema Benki hiyo na WFP wanafanya kazi kwa pamoja pia katika kutekeleza mradi wa 'shambani mpaka sokoni' ujulikanao kama Farm to Market Alliance (FTMA) ambapo mpaka sasa TADB imeweza kutoa mikopo inayofikia shilingi milioni 750 kwa vikundi nane vyenye wanachama 867 wanaolima jumla ya heka 2,789 Mkoani Ruvuma na Rukwa.

"Malengo ni kutafuta njia za kuimarisha FTMA na kuwanufaisha zaidi wakulima wadogo kupitia kwenye mfumo huu," ilisema taarifa hiyo.

Imeeleza kwamba wakati banki inashughulikia masuala ya fedha ambazo zinatumika kuhamasisha ubunifu kwenye kilimo vijijini, WFP kwa upande wake inahakikisha kwamba inakuwa chachu ya ubunifu huo.

Taasisi hizo pia zimekubaliana kutumia mbinu ambazo zitapunguza upotevu wa mazao kabla ya mavuno ili kuongeza mavuno nchini.

Taarifa hiyo ilifafanua kwamba kupitia mradi wa "Boresha Lishe" unaotekelezwa Singida na Dodoma, usalama wa chakula umeongezeka.

"Benki inataka kuhakikisha kwamba inafanya kazi kufanikisha uanzishwaji wa miradi ya kilimo yenye tija na kuongeza huduma za kifedha ili uwepo wake uwe na matunda kwa wananchi wote," ilieleza zaidi sema taarifa hiyo.

Katika kutekeleza mpango wa kuendeleza kilimo (ASDP II) unaosisitiza uwepo wa kilimo endelevu na usimamizi mzuri wa maji na ardhi, TADB inampango wa kufadhili angalau miradi 20 ya umwagiliaji, kuhamasisha matumizi ya tekinolojia kwenye umwagiliaji, kutoa pesa kwa ajili ya kituo cha mazao ya kilimo Kanda ya Ziwa na kutoa msaada wa kifedha kwa angalau miradi kumi inayohusika na utunzaji wa mazingira.




Meneja Mipango na Uendeshaji wa ABInBEV Afrika Mashariki, Nancy Riwa, akitoa mada wakati wa kongamano la wanawake jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kulia) ni Mkuu wa Mawasiliano na Uhusiano wa Vodacom Tanzania, Rosalynn Mworia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Prof. Ndalichako awapa shule wanafunzi wa kike

**Na Gurian Adolf,**
SUMBAWANGA

SERIKALI imewataka wanafunzi wa kike kujituma na kupata ufaulu mzuri katika mitihani ya taifa ili kunufaika na maboresho ya sekta ya elimu yanayoendelea kufanyika nchini.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wanafunzi wa kike wa kidato cha sita katika Shule ya Sekondari Kizwite mjini Sumbawanga ambao wanaanza mitihani yao ya kuhitimu kidato cha sita leo hii alipokuwa katika ziara yake ya kikazi mjini humo.

Alisema wanafunzi wa kike wana uwezo sawa na wanafunzi wa kiume, hivyo wanachopaswa kufanya ni kukazana katika masomo yao na mitihani ili kupata ufaulu mzuri.

Prof. Ndalichako alisema serikali imeboresha sekta ya elimu kuanzia shule za msingi, sekondari hadi elimu ya juu ili kila mtoto wa Mtanzania anufaike na maboresho hayo.

Alisema tangu serikali ya Rais John Magufuli ilipoingia madarakani imekuwa ikitoa elimu bure, kukarabati shule za sekondari, kuongeza kiwango cha wanafunzi wanaopata mikopo katika elimu ya chuo kikuu sambamba na kujenga mabweni kwa ajili ya wanafunzi hao.

"Natoa wito kwenu wanafunzi hususan wa kike kazaneni katika masomo ili muweze kupata ufaulu mzuri mnufaike na maboresho ambayo serikali imekuwa ikiyafanya kwa kuhakikisha inaweka mazingira mazuri ya elimu'," alieleza.

Aliwatakia kila la kheri katika mitihani hiyo na kuwataka kuondoa hofu kwa kuwa mitihani hiyo imeandaliwa kwa kuzingatia kile walichokisoma, hivyo ni matumaini yake kuwa ufaulu utaongezeka kwa kuwa wamejiandaa vizuri.

Mmoja wa wanafunzi, Flaviana Mosses, alisema wamejiandaa kikamilifu ili kunufaika na maboresho hayo, na aliishukuru serikali kwa jitihada kubwa inayofanya kuhakikisha inaboresha mazingira ya elimu na kutoa fursa ya elimu hata kwa watoto wa maskini kwa kutoa elimu bila malipo.


**Jipatie Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro kwa Bei Elekezi za Rejareja kama Ifuatavyo:-**

- **Nusu Lita (500ml) – TSHS. 500/=**
- **Lita Moja na Nusu (1.5L) – TSHS. 1,000/=**
- **Bei Hizi Elekezi ni Kwa Nchi Nzima**
- **Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro ni Maji ya Kuaminika Kila Siku**



# HABARI KITAIFA



Mama Maria Nyerere akiwa kwenye matembezi ya kuliombea taifa amani na maadhimisho ya Jubilee ya miaka 50 kwa Kituo cha Huduma ya Maombezi, Matembezi hayo yalifanyika juzi yalianzia Tazara ya kuishia Ubungo Riverside jijini Dar es Salam. **PICHA: BEATRICE MOSES**

## Bunge Afrika lajadili ubaguzi wa Waafrika Afrika Kusini

**Na Salome Kitomari**

KAMATI ya uongozi ya Bunge la Afrika (The Pan African Parliament Bureau), imekutana na mabalozi wanaowakilisha mataifa mbalimbali barani Afrika nchini Afrika Kusini kujadili na kutoa azimio kuhusu tabia ya ubaguzi wa waafrika maarufu kama Xenophobic nchini Afrika Kusini.

Kikao hicho kilifanyika mwishoni mwa wiki katika ukumbi wa Makao Makuu ya Bunge la Afrika kama sehemu ya mkutano wa maandalizi ya Mkutano wa Pili wa Bunge la Tano la Bunge la Afrika jijini Johannesburg, Afrika Kusini unaotarajiwa kuanza leo.

Akizungumza jana wakati wa mkutano huo wa mabalozi wa Afrika walioidhinishwa na Afrika Kusini, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Bunge la Afrika, Stephen Masele, alisema jambo hilo litajadiliwa kwa kina na kutoa maazimio.

"Suala hili linapaswa kuchukuliwa kwa umakini, kuna vitendo vya uhalifu vinavyofanywa na vikundi tofauti kutoka nje inaonekana kama Afrika Kusini haitaki wageni katika nchi yao...la hasha, lakini kwa undani kuna matendo ya uhalifu kwa kivuli cha Xenophobia," alisema Masele ambaye pia ni Mbunge wa Shinyanga Mjini.

"Ninafurahi na kuhamasishwa na hatua zilizochukuliwa na Serikali ya Afrika Kusini ili kukabiliana na mambo yote ya uhalifu.

Tutakuwa makini sana wakati tunajadiliana jambo hili kwa sababu hatutaki kuingilia kati mambo ya ndani ya Afrika Kusini au kuingilia kati vyombo vya usalama kutekeleza majukumu yao," alisema.

Masele aliomba mamlaka ya Afrika Kusini kushughulikia suala la tabia ya Xenophobic katika Afrika kwa kuwa haikubaliki.

"Sisi kama Wabunge wa Afrika tunatarajia kuona hatua kali zikichukuliwa dhidi ya wahalifu wote, wanaharibu sifa nzuri ya Afrika Kusini na Afrika. Bunge la Afrika litapaza sauti na kukemea suala hili...Vikwazo vya hali yoyote dhidi ya watu binafsi au nchi huumiza watu wasiokuwa na hatia hususani wanawake na watoto na huzuia jitihada za maendeleo za watu wetu na nchi hizo zina vikwazo," aliongeza.

Kikao cha pili cha kawaida cha Bunge la Tano la Bunge la Afrika kinatarajiwa kuanza mnamo Mei 6, mwaka huu, huko Midrand - jijini Johannesburg, Afrika Kusini.

Pamoja na mambo mengine watajadiliana kuhusu kaulimbiu ya Umoja wa Afrika ya mwaka huu "Mwaka wa Wakimbizi na Watu Waliopotea", pia Bunge la Afrika litajadili suluhisho la kudumu kuhusu tatizo la wakimbizi barani Afrika.

Aidha, Bunge pia litajadili taarifa kuhusu amani na usalama katika bara ikiwa ni pamoja na maendeleo ya hivi karibuni na hali ya kisiasa Libya, Sudan, Algeria na mchakato wa amani nchini Sudan Kusini.

Masele anahimiza pande zote zinazohusika katika majadiliano ya amani kuwa zisio na upendeleo kwa lengo la kutimiza ahadi zao kwa watu wa Afrika.


**KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

**JULIUS FAUSTINE SHIRIMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T. 460 BTH. TOYOTA.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **MB/RB/3907/2019.**

115212902


## Miaka 83 bila chuo cha serikali kukarabatiwa

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

CHUO cha Ualimu Vikindu Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, kinatoa elimu katika majengo chakavu ambayo hayajawahi kufanyiwa ukarabati kwa takribani miaka 83.

Inaelezwa kuwa pia nyumba za walimu nazo ni chakavu kutokana na kutokarabatiwa tangu mwaka 1936. Hayo yalibainishwa na mkuu wa chuo hicho, Amina Tou, wakati wa mahafali ya 18 ya chuo hicho.

Akisoma risala kwa mgeni rasmi, Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Sylivia Chinguwile, Tou alisema chuo hicho kilirithi majengo chakavu yaliyojengwa mwaka 1936, yaliyotumika kwa ajili ya Shule ya Msingi ya Kati.

"Toka kipindi hicho mpaka sasa ni miaka 83 majengo ni chakavu na hayajawahi kufanyiwa ukarabati," alisema.

Aliongeza chuo hicho ni miongoni mwa vyuo 35 vya serikali vinavyotoa mafunzo ya ualimu na kwamba kilianza kutoa mafunzo ya ualimu mwaka 1988. Kabla ya hapo kilikuwa Bagamoyo katika Chuo cha Uongozi wa Elimu (MANTEP, sasa ADEM).

Alisema mbali na uchakavu wa miundombinu, pia chuo hicho hakina gari, zahanati, maktaba, maabara pamoja na uhaba wa vyumba vya madarasa na mabweni.

Hata hivyo, aliishukuru serikali kwa kuwapatia kompyuta 30. Kwa upande wake, Chinguwile alisema ualimu ni wito, hivyo walimu wanatakiwa kuwa wabunifu katika ufundishaji.

Aliongeza kuwa changamoto za chuo wizara inazijua na inatarajia kuzitatua ikiwamo kuwaongeza kompyuta.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Stars kujipima na Misri haitoshi kuelekea Afcon

**WIKI** iliyopita Kocha wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Emmanuel Amunike, alitangaza kikosi chake kitakachoingia kambini mwezi ujao kwa ajili ya kujiandaa na fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon 2019) nchini Misri.

Katika fainali hizo zitakazoanza kutimua vumbi Juni 21, Stars imepangwa Kundi C pamoja na Algeria, Senegal na majirani zao, Kenya (Harambee Stars).

Ni dhahiri hili si kundi jepesi kwa Stars ambayo hii ni mara ya kwanza kushiriki fainali hizo tangu mwaka 1980 iliposhiriki kwa mara ya kwanza.

Hivyo, maandalizi ya kina yanahitajika ili kutotia aibu kwa kupoteza mechi zote kama ambavyo timu ya Taifa ya Vijana chini ya miaka 17 (Serengeti Boys), ilivyoitia nchi aibu katika michuano ya Afcon U-17 iliyomalizika hapa nchini mwezi uliopita.

Katika michuano hiyo, Serengeti Boys iliyokuwa Kundi A pamoja na Angola, Nigeria na jirani zao Uganda ilipoteza mechi zote licha ya kuandaliwa kwa muda mrefu kwa kucheza mechi nyingi za kirafiki na kushiriki mashindano mbalimbali ya kimataifa.

Kwa mantiki hiyo, kwa kuzingatia ukweli kwamba baadhi ya wachezaji wa Stars kutokuwa na uzoefu wa mechi za kimataifa huku wakicheza soka la ndani, tunaona ipo haja ya kupata zaidi ya mechi moja ya kujipima nguvu.

Stars itacheza mechi yake ya kwanza ya michuano ya Afcon Juni 23 dhidi ya Senegal kabla ya mchezo unaofuata kuivaa Uganda.

Tunatambua Senegal ni timu yenye wachezaji wengi wazoefu wa mechi za kimataifa na wanaocheza soka la kulipwa katika klabu kubwa Ulaya akiwamo mshambuliaji hatari anayeichezea Liverpool ya England, Sadio Mane.

Na katika kuelekea fainali hizo, tayari Shirikisho la Soka nchini (TFF) limetangaza kuwa Stars itaweka kambi Misri na kucheza mechi moja ya kirafiki dhidi ya wenyeji hao wa Afcon 2019. Tunaipongeza TFF kwa kufanikiwa kuitafutia Stars mechi hiyo ya kirafiki kwani tunatambua itakuwa ni jaribio nzuri kwa timu yetu hasa ukizingatia ukweli kwamba Misri nayo inaundwa na wachezaji wengi wazoefu wa mechi za kimataifa na baadhi wakicheza Ulaya.

Na si hilo tu, tunaamini kuwa safu ya ulinzi na idara nyingine zitapata nafasi ya kujifunza namna ya kumkaba Mane na wachezaji nyota wengine kwa kupitia Mohamed Salah anayecheza na Msenegal huyo kwenye Klabu ya Liverpool.

Pamoja na kufanikisha kupata mchezo huo wa kirafiki bado Nipashe tunaona ipo haja zaidi kwa TFF kuingia mawindoni na kuitafutia Stars mechi nyingine angalau mbili kabla ya kuanza kwa fainali hizo.

Kwa kufanya hivyo, si tu kutawasaidia wachezaji wa Stars kuendelea kujiimarisha, bali pia kutampa uwanja mpana kocha Amunike kupata kikosi cha kwanza na mifumo tofauti kulingana na aina ya wapinzani watakaokutana nao kwenye fainali hizo.


Tunaamini hilo linawezekana na lipo ndani ya uwezo wa TFF, na si lazima iumize kichwa sana kwani hata kama ikipata timu ambayo haipo kwenye fainali hizo, bado inaweza kuwa msaada kwa Stars na benchi lake ufundi katika maandalizi yao.

Aidha, wachezaji walioitwa Stars kujiandaa kwa fainali hizo, hawana budi kuanza maandalizi binafsi sasa na si kusubiri hadi watakapoingia kambini baadaye mwezi ujao.

Nipashe kama mdau namba moja wa soka nchini, tunataka kuona Stars ikipeperusha vema bendera ya Taifa na kuijengea Tanzania heshima katika medali ya soka kimataifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# TFF haijiamini, ilete waamuzi kutoka nje

**KWA** kawaida, binadamu anatakiwa aishi kwa kujiamini na kufanya kila kitu kwa utashi wake na si kwa kelele au maneno kutoka kwa watu wengine.

Ndiyo maana waswahili wanasema ishi unavyotaka wewe, usiishi wanavyotaka wao.

Nasema hili kwa kulilenga Shirikisho la Soka nchini (TFF), Bodi yake ya Ligi na Kamati ya Saa 72.

Inavyoonekana sasa imeanza kuendeshwa na mihemko ya watu kwenye mitandao ya kijamii, kuliko uhalisia.

Na kama ikiendelea hivi basi kuna hatari si soka la Tanzania kuwa la ajabu, lakini pia kuleta hata vurugu viwanjani.

Mara baada ya mechi ya kati ya Simba dhidi ya KMC kumalizika, mitandao ya kijamii ililipuka kuwashutumu waamuzi waliochezesha mechi hiyo, wakiongozwa na Abdallah Kambuzi kwa madai hawakuchezesha kwa haki.

Waamuzi hao walifungiwa si zaidi ya siku moja tu mara baada ya mechi hiyo. Wakati huo huo kuna baadhi ya adhabu au maamuzi yanatakiwa kutolewa mapema, lakini kumekuwa na ucheleshwaji mkubwa, lakini hili limetoka mapema sana kwa muda muafaka.

Sina nia ya kumtetea Kambuzi na wenzake, la hasha, lakini ukiangalia makosa yaliyofanywa kwenye mechi ile, hayatofautiani na makosa yaliyofanywa na waamuzi kwenye mechi zilizofuata kati ya Simba dhidi ya JKT Ruvu, Mbeya City dhidi ya Simba na hata Azam dhidi ya Yanga.

> **Sina nia ya kumtetea Kambuzi na wenzake, la hasha, lakini ukiangalia makosa yaliyofanywa kwenye mechi ile, hayatofautiani na makosa yaliyofanywa na waamuzi kwenye mechi zilizofuata kati ya Simba dhidi ya JKT Ruvu, Mbeya City dhidi ya Simba na hata Azam dhidi ya Yanga.**

Nadhani hawa waamuzi wamepona kwa sababu mitandao ya kijamii haikulipuka sana kama mechi ile ya Simba dhidi ya KMC, lakini ukiangalia mechi hizo utaona makosa mengi ya wazi ya waamuzi waliochezesha. Sasa unajiuliza kwa nini Kambuzi kaondolewa na wengine wameachwa. Au kwa sababu ni Kambuzi?

Baadhi ya waamuzi wa Tanzania kwa muda mrefu sana wamekuwa na matatizo makubwa kwenye uchezeshaji wa soka na hii haijaanza leo, jana wala juzi.

Na kama TFF kupitia vyombo vyake kama itataka kufuatilia mechi hadi mechi basi inaweza kujikuta inafungia mwamuzi mmoja au wawili kila wiki.

Acha Ligi Kuu, huko kwenye Ligi Daraja la Kwanza ndiyo usiseme, maana hadi timu ya Arusha United imejitoa kwa kulalamikia uonevu.

Kwa maana hiyo ni kwamba kama TFF kupitia Bodi ya Ligi au Kamati ya Saa 72 inataka kukomesha tabia mbaya ya waamuzi basi isisubiri watu walalamike na kucharuka kwenye mitandao ya kijamii, bali ichukue hatua stahiki.

Lakini ikiwa na tabia ya kuacha madudu na kusubiri watu walalamike na kutoa shutuma kwenye mitandao ya kijamii ndiyo wachukue hatua, hizo ni dalili za woga na kutojiamini kwenye majukumu yao.

Kitendo cha kumsimamisha mwamuzi Kambuzi ghafla hivi sasa kimeleta mambo mengi na hata waamuzi hivi sasa wamekuwa wakichezesha kwa woga.

Nimemsikia Kocha Mkuu wa Simba akisema kuwa baada ya mechi ile dhidi ya KMC, waamuzi wamekuwa wakiogopa kuipa haki ya penalti timu yake hata kama ni halali.

TFF na vyombo vyake kama inaona kuna waamuzi wanavurunda kwenye baadhi ya mechi na hawataki kulaumiwa kuwa kuna timu wanaibeba, nadhani sasa imefikia wakati wa kuwaita waamuzi kutoka nje ya nchi kuchezesha baadhi ya mechi kama wanavyofanya wenzetu Misri, Afrika Kusini, Congo DR, Morocco na kwingine.

Nafikiri waamuzi kutokana nje hata kama kutakuwa na makosa, basi mashabiki wataamini kuwa ni ya kibinadamu.

## TANGAZO

# YETU MICROFINANCE BANK PLC

Yetu Microfinance Bank PLC
"Creating Wealth Together, Pamoja Tunaweza"

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 MARCH 2019.
Kiwango kwa Tzs

| | | Robo Mwaka wa sasa 31-Mar-19 TZS | Robo Mwaka Ulipitia 31-Dec-18 TZS |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 386,677,366 | **375,447,532** |
| 2 | Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 255,549,507 | **107,999,019** |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | 0.00 | **0.00** |
| 4 | Salio katika Benki Nyinginezo na Taasisi za Fedha | 598,868,586 | **411,157,188** |
| 5 | Hundi na Miamala ya kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 0.00 | **0.00** |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0.00 | **0.00** |
| 8 | Dhima za Wateja zilizokubalika | 0.00 | **0.00** |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 0.00 | **0.00** |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0.00 | **0.00** |
| 11 | Mikopo Halisi iliyopo | 12,404,698,002 | **12,939,962,781** |
| 12 | Mali Nyingine | 1,074,999,616 | 1,277,632,358 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | | |
| 14 | Akaunti za udhamini | 0.00 | **0.00** |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | **725,447,130** | **704,497,292** |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **15,446,240,206** | **15,816,696,169** |
| B. | **DHIMA** | **0** | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | | |
| 18 | Amana za Wateja | **1,581,007,686** | **1,110,559,271** |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | **0.00** | **0.00** |
| 20 | Amana Maalumu | **1,585,187,087** | **1,688,328,257** |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | **0.00** | **0.00** |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | **0.00** | **0.00** |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | **0** | **0** |
| 24 | Dhima la Tozo kwa ajili ya usuluhishi baina ya Benki na Mte | **0.00** | **0.00** |
| 25 | Miamala isiyoshughulikiwa baina ya Matawi | **0.00** | |
| 26 | Mapato yalioingia ya kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa baadae | | |
| 27 | Dhima Nyingine | **627,098,343** | **129,024,082** |
| 28 | Madeni | **3,700,000,000** | **4,000,000,000** |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **7,493,293,116** | **6,927,911,610** |
| 30 | **MALI/{DHIMA} HALISI** | **7,952,947,090** | **8,888,784,559** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Ulioliрwa | **6,056,496,547** | **6,056,496,547** |
| 32 | Akiba ya Mtaji | **0** | **0** |
| 33 | Mapato yaliyobakizwa | **-** | **-** |
| 34 | Faida/{Hasara} ya Kipindi Husika | **1,512,555,000** | **2,293,869,509** |
| 35 | Akaunti zingine za Mtaji | **276,730,778** | **298,103,133** |
| 36 | Stahiki ya wenye Hisa chache | **107,164,765** | **240,315,370** |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **7,952,947,090** | **8,888,784,559** |
| 38 | Dhima zisizo dhahiri | **0** | **0** |
| 39 | Mikopo chechefu | **723,403,220** | **863,289,239** |
| 40 | Tengo Kwa ajili ya mikopo chechefu | **831,397,072** | **1,001,343,399** |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | **0.00** | **0.00** |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | **%** | **%** |
| i | Uwiano wa Fedha za wanahisa na Jumla ya Mali | 51% | 56% |
| ii | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 5% | 6% |
| iii | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | **418%** | **498%** |
| iv | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 80% | 82% |
| v | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 84% | 84% |
| vi | Ongezeko la Amana | **42%** | 18% |
| vii | Ongezeko la Mali | **2%** | **54%** |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA ULIOISHIA 31 MACHI 2019.
Kiwango kwa Tzs.

| | | Robo Mwaka wa sasa 31-Mar-19 TZS | Robo Mwaka Ulipitia 31-Dec-18 TZS | Limbikizo Robo Mwaka wa sasa 31-Mar-19 TZS |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 1,274,548,605 | 1,289,161,932 | 1,274,548,605 |
| 2 | Gharama za Riba | 87,397,260 | 87,808,219 | 87,397,260 |
| **3** | **Mapato Halisi (1 kutoa 2)** | **1,187,151,345** | **1,201,353,712** | **1,187,151,345** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | | | |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika mikopo | 169,946,327 | 15,577,003 | 169,946,327 |
| **6** | **Mapato yasiyo ya Riba:** | **165,079,650** | **207,035,546** | **165,079,650** |
| | 6.1 Faida/(Hasara) zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | | | |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 138,799,029 | 164,998,739 | 138,799,029 |
| | 6.3 Gawio | | | |
| | 6.4 Mapato Mengine | 26,280,620 | 42,036,807.29 | 26,280,620 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **1,153,202,951** | **1,039,709,123** | **1,153,202,951** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 359,224,220 | 394,263,950 | 359,224,220 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | | | |
| | 7.3 Gharama nyingine | 793,978,731 | 645,445,173 | 793,978,731 |
| 8 | **Faida/(Hasara) ya Uendeshaji** | **368,974,371** | **384,257,139** | **368,974,371** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 92,243,593 | 55,000,000 | 92,243,593 |
| 10 | **Faida/(Hasara ) Halisi baada ya Kodi ya Mapato** | **276,730,778** | **329,257,139** | **276,730,778** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa{bainisha} | | | |
| 12 | **Jumla ya Faida/{Hasara} iliyojumuishwa kwa Mwaka** | **276,730,778** | **298,103,133** | **276,730,778** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | **125** | 125 | 125 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | **30.00** | 29.00 | 30.00 |
| 15 | Idadi ya Matawi | **3** | 3 | 3 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | **15%** | 15.20% | **15%** |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | **20%** | 19.80% | **20%** |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | **85%** | 74.00% | **85%** |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | **15%** | 15.00% | **15%** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI 2019
Kiwango kwa Tzs

| | | Robo Mwaka wa sasa 31-Mar-19 TZS | Robo Mwaka Liganishi 31-Dec-18 TZS |
|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **368,974,371** | **353,103,133** |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | | |
| | - Faida/{Hasara} kwenye Mauzo ya Mali | | |
| | -Uchakavu wa Mali za Kudumu | **41,320,630** | 40,010,365 |
| | -Uchakavu wa Matengenezo Makubwa | | |
| | -Utumikaji wa Mtaji wa Misaada | **-** | **-** |
| | -Uchakavu wa Mali Zisizoshikika | | |
| | | **368,974,371** | **353,103,133** |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Salio la Benki Kuu ya Tanzania | **-** | **-** |
| | - Badiliko Halisi katika Mikopo | **(535,264,779)** | (7,493,671) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | **-80,001,367** | (316,053,236) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | **470,448,415** | 105,209,544 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika salio la benki Nyingine na Taasisi za Fedha | **(103,141,170)** | (254,955,606) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | **498,074,261** | (93,511,071) |
| | | **619,089,731** | **(213,700,907)** |
| | - Kodi Iliyolipwa | (43,500,000) | (55,000,000) |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **616,910,361** | **(228,690,542)** |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| | Gawio Lililopokewa | | |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (20,418,643) | (56,021,935) |
| | Mapato kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 0.00 | 0.00 |
| | Ununuzi wa Mali Zisizoshikika | 50,000,000 | 50,000,000 |
| | Mengineyo Amana za kudumu | | |
| | Mapato kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | | |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa*** | **29,581,357** | **(6,021,935)** |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | (300,000,000) | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | | |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | | |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | (2,357,093) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha* | **(300,000,000)** | **(2,357,093)** |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| | Ongezeko/ Punguzo Halisi katika Fedha taslimu na Mali zinazofanana na Fedha | **346,491,718** | **(237,069,570)** |
| | Fedha na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | **894,603,739** | **1,131,673,309** |
| | Fedha na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka | **1,241,095,458** | **894,603,739** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 MARCH 2019
Kiwango kwa Tzs.

| Kiwango kwa Tzs.'(000)' | Mtaji wa Hisa | Mtaji mkuu wa kisheria | Mtaji wa kisheria | | Akaunti zingine za Mtaji | Tengo la ziada ya juma | Jumla Tzs |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Salio la wa mwaka 01/01/2018 | 6,056,497 | 124,847 | 66,617 | - | 157,165 | 1,522,511 | 7,927,637 |
| Rekebisho : | | | | | | - | - |
| Ongeza: Jumlisha/(Futa) kwa kipindi cha robo | - | - | - | - | (50,368) | - | (50,368) |
| Mapato mengine | | | | | (37,104) | | (37,104) |
| Mtaji mkuu wa kisheria | | 5,708 | | | | (5,708) | - |
| Mtaji wa kisheria | | | (66,617) | | | 66,617 | - |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya kodi ya mapato | - | - | - | - | - | 709,126 | 709,126 |
| Gawio lililolipwa | | | | | | (779,900) | (779,900) |
| **Salio kwa robo 31.12.2018** | **6,056,497** | **130,555** | **-** | **-** | **69,693** | **1,512,646** | **7,769,391** |
| **Salio la mwaka 01.03.2019** | **6,056,497** | **130,555** | **-** | **-** | **69,693** | **1,512,646** | **7,769,391** |
| Rekebisho : | - | | | | | | - |
| Ongeza: Jumlisha/(Futa) kwa kipindi cha robo | - | | | | 37471 | | 37,471 |
| Toa: Mapato mengine | - | | | | 0 | 0 | - |
| Mtaji wa kisheria | - | | - | - | | - | - |
| | - | | | - | | 0 | - |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya kodi ya mapato | - | | | | | 276,731 | 276,731 |
| Toa: Gawio lililotolewa | - | | | | | - | - |
| **Salio kwa mwaka 31.03.2019** | **6,056,497.0** | **130,555.0** | **-** | **-** | **107,164.0** | **1,789,377.0** | **8,083,593.0** |

### ADA NA GHARAMA ZA HUDUMA

AINA YA BIDHAA

| 1. AKAUNTI ZA AKIBA | | 2. Mkopo | |
|---|---|---|---|
| Kima cha chini cha kufungua akaunti | 5000/= | Mikopo ya biashara | 3% pm |
| Ada ya mwezi | BURE | Mikopo ya kuboresha nyumba | 1.4% pm |
| Taarifa ya Akaunti | BURE | Ada ya Mkopo | 1.80% |
| Kuuliza salio | BURE | Bima ya mkopo | 1.68% |
| Kufunga akaunti | 5000/= | Mikopo ys Jikimu | 1.5% pm |
| Gharama za kuendesha akaunti | 5000/= | Agricultural Loan | 1.4% pm |
| Gharama za kuweka fedha | BURE | Mikopo ya kulipia Bima ya afya | 2.3% pm |
| Account maintanance charge | FREE | | |
| Account maintanance charge | FREE | | |

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| **Imesainiwa na:** | **Cheo** | **Tarehe:** |
|---|---|---|
| ***Altemius Millinga*** | ***Mkurugenzi Mtendaji*** | ***2-Mei-2019*** |
| ***Samwel Gikaro*** | ***Meneja wa Fedha*** | ***2-Mei-2019*** |
| ***Angela Fanuel*** | ***Mkaguzi wa Ndani*** | ***2-Mei-2019*** |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| ***Kuthibitishwa na:*** | | |
|---|---|---|
| ***Ernest K. Ndimbo*** | ***Mwenyekiti wa Bodi*** | ***2-Mei-2019*** |
| ***Happy sambega*** | ***Mkurugenzi*** | ***2-Mei-2019*** |

# Barabara ya mwisho ya Dk. Mengi

INATOKA UK. 2

ya Jumanne ambayo utaagwa katika viwanja vya Karimjee na siku ya Jumatano utakaposafirishwa kuelekea Machame wilayani Hai Mkoa wa Kilimanjaro kwa maziko siku ya Alhamisi.

Makonda alisema katika ratiba hiyo ya siku tatu, uongozi wa mkoa huo, unashirikiana na wanafamilia kuhakikisha ratiba hiyo inaenda kama ilivyopangwa.

"Tumejipanga uongozi wa mkoa kwa kushirikiana na familia kuupokea mwili wa Dk. Mengi na kuupeleka Lugalo, siku ya pili ibada na kuuaga pale Karimjee na siku ya tatu kuusindikiza uwanja wa ndege kwa ajili ya kuelekea mkoani Kilimanjaro," alisema Makonda.

Aliwasihi Watanzania na wananchi wa mkoa huo ambao wameguswa na msiba huo, siku ya kumuaga iwe ya kusherehekea na kumshukuru Mungu kwa maisha ya Dk. Mengi kwa sababu amekuwa kuwa sikio la watu waliokata tamaa na kuwainua wasiojiweza.

Alisema Dk. Mengi alikuwa akipaza sauti za watoto wa mitaani, yatima, walemavu na wasiyo na uwezo na alijitoa bila kujali kuwa atapata chochote kutoka kwao.

Alisema Dk. Mengi alikuwa na mchango mkubwa katika sekta zote muhimu kama michezo, biashara, mazingira na kuajiri Watanzania wengi.

"Ukimuongelea Dk. Mengi kwenye uadilifu na kupiga vita rushwa utamkuta na amewapigania walemavu wengi nchini. Kwa ufupi, ni mzee wa kwanza wa kichaga niliyemfahamu ambaye alikuwa anatoa fedha zake kusaidia wengine bila kusubiri malipo. Hakuwa mchungu kutoa fedha yake na alifanya hivyo bila kuwa na ndoto ya kugombea chochote, bali kwa moyo wa upendo," alisema zaidi.

Alisena nchini wapo watu wenye moyo wa kusaidia, lakini kwa malengo ya kunufaika na misaada wanayotoa kama kugombea nafasi za uongozi tofauti na alivyokuwa Dk. Mengi.

Makonda alieleza zaidi: "Kwa upendo ambao Dk. Mengi aliuonyesha kwa Watanzania wengi kama shujaa wetu na sikio la watu waliokata tama, tujitokeze kwa wingi kusherehekea maisha yake."

Makonda aliendelea kusema kuwa Dk. Mengi alikuwa mtu ambaye hakukubali kukatishwa tamaa na mazingira.

Alisema licha ya kuwa, alikuwa tayari ameshafikisha miaka 75, alikuwa na ndoto ya kuanzisha kiwanda kikubwa cha magari Tanzania na kuanzisha kiwanda cha dawa.

Alisema kwake yeye binafsi mbali na kumpatia msaada wa masomo, alikuwa mtu aliyemfanya kama baba yake, kiongozi na mshauri wa mambo mengi ya msingi.

"Ni mtu mwenye upendo wa hali ya juu na hata nilipopata mtoto alikuwa mfanyabiashara mkubwa wa kwanza kuja kwangu na kunipa hongera na kufanya ibada ya maombi nyumbani kwangu na familia yangu, ni kitu ambacho kilinifanya nimuone mwenye upendo wa hali ya juu," alisema Makonda.

Alisema kwa sababu alikuwa ni tajiri angeweza kumpatia zawadi aliyoitaka kumpatia bila kwenda, lakini alienda nyumbani kwake na kumfanyia maombi na kuwapa ushauri.

"Nimempoteza baba mlezi, mshauri na kiongozi ambaye alikuwa na upendo wa hali ya juu kwa watu wote," alisema Makonda.

# ...Wengi waendelea kumlilia Dk. Mengi

INATOKA UK. 2

"Mwaka 2002 tukakutana Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) tukiwa wote tumealikwa tukazungumze na wanafunzi ndoto yangu ya mwaka 1998, akanikaribisha ofisini kwake na hapa nyumbani nimekuja mara nyingi, huyu mzee amekuwa mwema tangu nimemfahamu hadi anakufa," alisema.

Alisema ingawa alikuwa mshindani wake kwenye biashara, lakini alikuwa anamshauri namna ya kufanya ili aweze kufanikiwa.

**FRANCIS NANAI**

Mkurugenzi wa Mwananchi Communications (MCL), Francis Nanai, alisema Dk. Mengi alikuwa kiongozi ambaye anatambulika Afrika kwa kazi na uwekezaji alioufanya.

"Tumepoteza mtu ambaye alikuwa muhimu kwetu, watu wazuri wameumbwa kwa sababu, na sababu ikikamilika Mungu huwachukua, tunashukuru kwa maisha aliyoyaishi amekuwa mfano mzuri kwetu, ameacha deni kubwa kwetu, hapo alipoishia je, tunaweza kupaendeleza?" alihoji.

Nanai alisema alimfahamu Dk. Mengi tangu alipomaliza Chuo Kikuu na kuajiriwa Kampuni ya Coca Cola.

**SALMA KIKWETE**

Mke wa Rais Jakaya Kikwete, Salma Kikwete alisema Dk. Mengi alikuwa mtu jasiri, alisimamia kile anachokiamini na alikuwa msaada mkubwa kwa Watanzania wote bila kujali dini, kundi rika kwenye jamii.

"Binafsi nitamkumbuka, naona mwenyezi Mungu alitaka iwe hivyo, wakati akielekea Zanzibar aliongea na mume wangu walivyozungumza nami niliongea naye.

"Akaniambia mama kuna jambo tuliongea lile jambo litakuwa endelevu? akaniuliza Katibu ni yule yule Daudi nikamwambia Ali Jakaya Kikwete, akanisisitiza jambo," alisema.

**HAWA GHASIA**

Mbunge wa Mtwara Vijijini (CCM), Hawa Ghasia, alisema Dk. Mengi ni miongoni mwa wafanyabiashara waliotusaidia wabunge wanawake wenye majimbo.

**BINTI MWENYE ULEMAVU**

Naye, Wakonta Kapunda, msichana anayeandika kwa ulimi baada ya kupooza kutoka shingoni kwenda chini alisema Dk. Mengi alikuwa mtu mwenye moyo mzuri, mwenye mapenzi na kujali kila mtu.

Binti huyo ambaye aliwahi kujishindia fedha taslimu kupitia shindano la Dk. Mengi baada ya kuandika wazo zuri la biashara alisema fedha hizo zimemsaidia na biashara zinaendelea vizuri. "Dk. Mengi ukikaa naye haongelei kuhusu biashara, anaongelea jinsi gani ya kutatua matatizo yaliyopo kwenye jamii, jinsi gani ya kuondoa umaskini, yeye muda wote alikuwa anaangalia changamoto, ukisoma kitabu chake utagundua kila mafanikio ya biashara zake imetokea kwenye kutatua tatizo," alisema.

**HECHE SUKUTA**

Mwanasheria wa Baraza la Taifa la Mazingira (Nemc), Heche Sukuta,alisema Dk. Mengi alikuwa Mwenyekiti wa bodi ambaye aliongoza katika mabadiliko ya kisera na muundo na kujenga weledi wa kimkakati ili mazingira yalindwe.

Viongozi wengine waliofika nyumbani kwa Dk. Mengi jana ni Makamu wa Rais mstaafu, Dk. Mohamed Gharib Bilal, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Bernard Membe na Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Humphrey Polepole.

# Ajeruhiwa na simba

INATOKA UK. 3

eneo hilo na kuanza kumshambulia na kupata majeraha katika tumbo na kifua, alipopiga kelele za kuomba msaada kutoka wka majirani, wanyama hao walikimbia na kumuacha Kizoto akivuja damu.

Alisema wasamaria wema walipofika eneo la kibandani walimkuta kaka na kumchukua hadi kituo kidogo cha Polisi Kata ya Rutamba na kupatiwa Fomu ya PF3 na kumkimbiza Kituo cha Afya cha Rondo, lakini kutokana na ukubwa wa tatizo hilo, Mganga wa Kituo hicho, aliamuru apelekwe Hospitali ya Sokoine.

"Ninashukuru Mungu tangu tumefika hapa tumepokelewa vizuri na watumishi wa hapa hospitali na kumpatia huduma za matibabu," alisema Michael.

Mmoja wa watumishi wa Hospitali hiyo, Dk. Ernest Mhando, alisema wamempokea majeruhi Kizito akiwa na majeraha kati ya kifua na tumboni, kulikochangiwa na kushambuliwa kwa kucha za simba, na walipompokea walimuanzishia matibabu haraka na hali yake inaendelea vizuri.

Afisa Maliasili wa Wilaya ya Lindi, Victor Shau, aliwashauri wananchi wanaoishi maeneo yanayokaribiana na Msitu wa Tarafa ya Rondo kuchukua taadhali ikiwamo kutotembea ovyo nyakati za usiku kutoka kijiji kimoja kwenda kingine ili kulinda usalama wa maisha yao.

# Hiace ilivyoua 10, kujeruhi 12

INATOKA UK. 3

Joseph alisema walipokea maiti 8 na majeruhi 12, wawili kati ya hao walifariki dunia na mmoja wa majeruhi alifariki akiwa chumba cha dharula.

Aliongeza kuwa mmoja alifariki wakiwa wanajaribu kuokoa maisha katika chumba cha upasuaji, hivyo waliofariki dunia kwa ajali hiyo kufikia 10.

Aidha, alisema mmoja kati ya majeruhi alikuwa ni mtoto wa miezi 3 ambaye amelazwa wodi ya watoto kwa ajili ya kumtunza wakati wakiendelea kumtafuta mzazi wake.

Alisema majeruhi waliosalia katika hospitali hiyo ambao wanaendelea na matibabu wodi namba saba ni majeruhi saba ambao ni wanaume na wodi namba tano majeruhi wawili ambao ni wanawake na mtoto mmoja, na kwamba na hali zao zinaendelea vizuri.

Kwa upande wake majeruhi Baraka Athumani (31), mkazi wa Kijiji cha Kalenge, alisema alikuwa abiria katika basi hilo na alikuwa akitokea kijiji cha Kalenge kuelekea Kigoma.

Alieleza kuwa gari hilo lilikuwa katika mwendo mkali kwa sababu lilikuwa linakimbizana na gari lingine, na kuwa ilipofika Kijiji cha Murela ikapinduka kwa sababu taili ya nyuma ilipasuka.

Athumani alisema ilipotokea ajali hiyo alipoteza fahamu na alizinduka akiwa wodi namba 7 katika Hospitali ya Rufaa ya Maweni na amevunjika miguu yote na mkono wa kulia pamoja na jeraha kwenye paji la uso.

# 91,442 kidato cha 6 kufanya mitihani leo

INATOKA UK. 2

Alisema kati ya watahiniwa wa kujitegemea 11,117 waliosajiliwa, wanaume ni 7,190 sawa na asilimia 64.68 na wanawake ni 3,927 sawa na asilimia 35.32.

Alisema watahiniwa wa kujitengemea wenye uoni hafifu ni 15 ambapo kwa mwaka jana idadi yao ilikuwa ni 10,421.

Dk. Msonde alisema jumla ya watahiniwa 12,540 wamesajiliwa kufanya mtihani wa kozi za ualimu.

"Kati yao 7,594 ni ngazi ya Stashahada na 4,946 ni ngazi ya Cheti. Kati ya watahiniwa 7,594 wa ngazi ya Stashahada waliosajiliwa, 5,615 sawa na asilimia 74 ni wanaume na 1,979 sawa na asilimia 26 ni wanawake," alisema.

Pia alisema kati ya watahiniwa 4,946 wa ngazi ya Cheti waliosajiliwa, 2,795 sawa na asilimia 57 ni wanaume na 2,151 sawa na asilimia 43 ni wanawake.

Alisema kwa mwaka jana idadi ya watahiniwa wa ngazi ya ualimu waliosajiliwa walikuwa ni 7,422, hivyo kuna ongezeko la jumla ya watahiniwa 5,118 sawa na asilimia 41 kwa mwaka huu.

Alisema maandalizi ya mitihani hiyo yamekamilika ikiwa ni pamoja na kuisambaza, vijitabu vya kujibia na nyaraka zote muhimu zinazohusu mitihani hiyo katika mikoa yote Tanzania Bara na Visiwani.

Dk. Msonde alisema kuwa mitihani hiyo ina umuhimu kwa sababu hupima maarifa, stadi za umahiri wa mwanafunzi katika yale aliyojifunza kwa kipindi cha miaka miwili ya sekondari ya juu.

"Baraza linatoa wito kwa Kamati za Mitihani za mikoa na Halmashauri, Manispaa na Jiji kuhakikisha kuwa taratibu zote za uendeshaji mitihani ya taifa zinazingatiwa ipasavyo," alisema.

Alizitaka kamati hizo zihakikishe kuwa mazingira ya vituo vya mitihani yapo salama, utulivu na kuzuia mianya yote itakayowezesha kusababsisha kutokea kwa udanganyifu.

"Baraza linatoa wito kwa wasimamizi wote kufanya kazi yao kwa umakini na uadilifu wa hali ya juu. Wasimamizi wanaelekezwa kufanya kazi yao kwa weledi na kuzingatia kanuni za mitihani na miongozo waliyopewa," alisema.

Alisema Baraza liliwakumbusha wasimamizi hao kuwa haki hizo ni pamoja na kuwapa mitihani yenye maandishi ya nukta nundu kwa watahiniwa wasioona na maandishi yaliyokuzwa kwa watahiniwa wenye uoni hafifu.

"Watahiniwa wote wenye mahitaji maalum waongezewe muda wa dakika ishirini kwa kila saa kwa somo la Hisabati na dakika kumi kwa kila saa kwa masomo mengine,kama mwongozo wa Baraza unavyoelekeza," alisema.

Pia limewataka wasimamizi wa mitihani, wamiliki wa shule, walimu na wanachi kutojihusisha na vitendo vyovyote vya udanganyifu wa mitihani hiyo.

Aidha, Baraza hilo limewaomba wadau wote kutoa taarifa katika vyombo husika kila wanapobaini uwepo wa mtu au kikundi cha watu kujihusisha na udanganyifu wa mitihani hiyo.

## TANGAZO


WIZARA YA MAJI
WAZIRI WA MAJI
Mhe. Prof. Makame Mbarawa (Mb)
NAIBU WAZIRI
Mhe.Jumaa Aweso (Mb)
KATIBU MKUU
Pro. Kitila Mkumbo
NAIBU WAZIRI MKUU
Mhandisi Emmanuel N.M. Kalobelo
HOTUBA YA MAKADIRIO
YA MAPATO
NA MATUMIZI YA WIZARA YA
MAJI KWA MWAKA
2019/20

# Muhtasari wa Hotuba ya Waziri wa Maji, Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa (Mb), wakati akiwasilisha Bungeni makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Wizara ya Maji kwa Mwaka 2019/2020

Tarehe 2 Mei, 2019 Waziri wa Maji, Mhe. Profesa Makame Mbarawa (Mb), aliwasilisha bajeti ya Wizara ya Maji katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hotuba ya Bajeti imegawanyika katika maeneo makubwa saba, ambayo ni **Mabadiliko ya Mfumo katika Uendeshaji wa Sekta ya Maji; Hali ya Sekta ya Maji nchini; Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka 2018/2019; Utekelezaji wa Miradi ya Maji kwa Mwaka 2018/2019; Baadhi ya Miradi Mipaya itakayotekelezwa katika Mwaka 2019/2020; Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka 2019/2010; na Hitimisho na Shukrani.**

Muhtasari huu, unaainisha maeneo muhimu ya hotuba ili umma uweze kuelewa namna Bajeti ya Mwaka 2018/2019 ilivyotekelezwa, mipango na vipaumbele vya Serikali katika utatuzi wa changamoto za utunzaji wa rasilimali za maji na upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama ya kunywa na matumizi mengine katika Bajeti ya Mwaka 2019/2020.

## 1.Mabadiliko ya Mfumo katika Uendeshaji wa Sekta ya Maji

Katika mwaka wa fedha wa 2018/2019, mabadiliko mawili ya kimfumo yalifanyika katika Sekta ya Maji. Mosi, muundo wa Wizara ya Maji ulibadilika katika maeneo makubwa mawili. Kwanza ni kuondolewa kwa Sekta ya Umwagiliaji katika **Wizara ya Maji** na kuhamishiwa Wizara ya Kilimo. Kufuatia mabadiliko haya, jina la Wizara ya Maji lilibadilika kutoka Wizara ya Maji na Umwagiliaji na hivi sasa jina ni Wizara ya Maji. Pili, ni kuunganishwa kwa Idara mbili za Usambazaji Maji zilizokuwepo awali, yaani Idara ya Usambazaji Maji Mijini na Idara ya Usambazaji Maji vijijini na kuunda idara moja inayoitwa Idara ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira. Sanjari na hatua hii, kuanzishwa kwa kitengo kipya ndani ya idara hii ambacho kitashughulikia masuala ya usafi wa mazingira. Kitengo hiki kinaongozwa na Mkurugenzi Msaidizi.

Pili, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilitunga sheria mpya ya huduma ya maji: **Sheria Na. 5 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2019.** Pamoja na mambo mengine, sheria hii imeanzisha **Wakala ya Maji Vijijini (Rural Water Supply and Sanitation Agency-RUWASA).** Kutungwa kwa sheria hii ni sehemu ya utekelezaji wa maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyoyatoa tarehe 10 Mei, 2018. Katika maelekezo yake, Mheshimiwa Rais aliagiza, pamoja na mambo mengine, kuwa watumishi wote wa Sekta ya Maji nchini wasimamiwe na Wizara ya Maji. Kufuatia kutungwa kwa Sheria mpya ya Huduma za Maji, watumishi wote wa Sekta ya Maji nchini watasimamiwa na Wizara ya Maji. Kwa hiyo, watumishi wa Sekta ya Maji waliokuwa chini ya Halmashauri za Wilaya/Miji/Manispaa/Majiji na Sekretariati za Mikoa sasa watahamishiwa Wizara ya Maji na watakuwa chini ya Wakala ya Maji Vijijini (RUWASA). Tayari Waziri wa Maji ameshatangaza kuanzia tarehe 1 Julai, 2019 kutumika kwa sheria mpya na kuanza kufanya kazi wa Wakala ya Maji Vijijini.

Kuanzishwa kwa Wakala ya Maji Vijijini kunatarajiwa kuboresha usimamizi wa Sekta ya Maji Vjijini, hususan katika ukamilishaji na uendelevu wa miradi ya maji vijijini.

## 2. Hali ya Sekta ya Maji

Sekta ya Maji nchini hupimwa kwa kuangalia vigezo vitatu; kwanza ni kiwango cha rasilimali za maji kinachopatikana katika nchi. Hadi mwezi Machi mwaka huu, inakadiriwa kuwa rasilimali za maji zinazofaa kwa matumizi mbalimbali nchini ni wastani wa **mita za ujazo bilioni 126** kwa mwaka, zikijumuisha **mita za ujazo bilioni 105** juu ya ardhi na mita za ujazo bilioni 21 chini ya ardhi. Matumizi yote ya maji kwa sasa nchini yanakadiriwa kuwa **mita za ujazo bilioni 40,** ambazo ni sawa na asilimia 31.7 ya maji yote yanayofaa kwa matumzi ya binadamu.

Kwa wastani, kiwango cha maji kwa mtu nchini ni sawa na mita za ujazo 2,300 (au mapipa 11,500) kwa mwaka. Kiwango hiki ni juu kidogo ya kiwango cha chini cha kimataifa cha mita za ujazo 1700 kwa mwaka ambacho chini ya hapo nchi huonekana kuwa ina uhaba wa maji. Hata hivyo, ni wazi kuwa mahitaji ya maji yanazidi kuongezeka kutokana na ongezeko la idadi ya watu kwani mwaka 1962 wastani wa maji kwa mtu kwa mwaka ilikuwa ni mita za ujazo 7,862 (mapipa 39,310). Hivyo ni muhimu kama taifa tuendelee kulinda vyanzo vya maji ili nchi iendelee kuwa na maji ya kutosheleza kwa vizazi vijavyo.

Pili, maendeleo ya sekta ya maji hupimwa kwa kuangalia kiwango cha ubora wa maji ambacho hutofautiana kulingana na hali ya kijiografia ya eneo husika, hali ya miamba ya asili na shughuli za binadamu. Tafiti zinaonyesha kuwa kwa maeneo mengi ya Tanzania changamoto za ubora wa maji juu ya ardhi ni uwepo wa Nitrogen, Phosphorous na tope katika maji. Kwa upande wa maji juu ya ardhi, changamoto ni uwepo wa kiwango kikubwa cha chumvichumvi, Nitrate, madini ya Flouride, Chuma, Manganese na Chloride. Vipimo vilivyochukuliwa katika vyanzo mbalimbali vya maji vinaonyesha kuwa hali ya ubora wa maji katika vyanzo mbalimbali vya maji inaridhisha na vinaweza kuendelezwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali baada ya kutibiwa na kuwa salama kulingana na matumizi yaliyokusudiwa.

Tatu, maendeleo ya sekta ya maji hupimwa kwa kuangalia kiwango cha usambazaji wa maji kwa matumizi mbalimbali, kipaumbele kikubwa kikiwa ni maji safi na salama ya kunywa. Kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2002, wananchi wanapaswa kupata huduma ya maji ya kunywa ndani ya **mita 400**. Kwa upande wa vijijini, huduma ya maji hutolewa kupitia vituo vya maji ambapo kituo kimoja kinapaswa kuhudumia watu wasiozidi 250. Kupitia Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2015, pamoja na miongozo mbalimbali ya kisera, serikali imeweka lengo la kufikisha maji kwa angalau **asilimia 85** kwa upande wa wananchi waishio vijijini, na **asimilia 95** kwa upande wa wananchi waishio mijini ifikapo mwaka 2020.

# TANGAZO

Hadi kufikia mwezi Aprili 2019, jumla ya miradi ya maji **1,659** yenye vituo vya kuchotea maji **131,370** ilijengwa. Kati ya vituo vilivyojengwa, vituo 86,780 vinafanya kazi na vina uwezo wa kuhudumia wananchi wapatao **25,359,290** sawa na **asilimia 64.8** ya wananchi waishio vijijini. Kwa takwimu hizi wastani wa wananchi wanaopata maji vijijini ni **asilimia 65 (64.8%).** Hii inamaanisha kuwa takribani vituo **44,590 (33.9%)** havifanyi kazi ikiashiria kuwa kuna changamoto kubwa katika uendelevu wa maji vijijini. Changamoto hii inaendelea kushughulikiwa na wizara kwa kuchukua hatua mbalimbali, ikiwemo kuanzishwa kwa Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) itakayokuwa na jukumu la kusimamia ujenzi na ukarabati wa miradi ya maji vijijini.

Huduma ya maji katika maeneo ya mijini hutolewa na Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Miji Mikuu ya Mikoa, Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na maeneo yanayohudumiwa na Miradi ya Kitaifa. Malengo ya Serikali ni kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Miji Mikuu ya Mikoa kufikia **asilimia 95;** na Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa kufikia **asilimia 90** ifikapo mwaka 2020. Kwa upande wa huduma ya uondoaji wa majitaka, lengo la Serikali ni kuongeza huduma hiyo hadi kufikia asilimia 30 ifikapo mwaka 2020.

Hadi kufikia mwezi Aprili 2019, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo yanayohudumiwa na Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Miji Mikuu ya Mikoa ilikuwa **asilimia 80** na kwa Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa upatikanaji wa huduma hiyo ilikuwa **asilimia 64.** Aidha, kwa upande wa huduma ya uondoaji majitaka katika maeneo ya mijini, hadi kufikia mwezi Aprili 2019, huduma hiyo imefikia wastani wa **asilimia 20** kwenye miji yenye mtandao wa majitaka.

## 3. Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2018/2019

Katika mwaka 2018/2019, Wizara ya Maji iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya **Shilingi bilioni 697. 57** na kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 24.363** zilikuwa ni fedha za matumizi ya kawaida na **Shilingi bilioni 673.214** zilikuwa ni fedha za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili 2019, jumla ya **Shilingi bilioni 16.653** sawa na **asilimia 68** za matumizi ya kawaida zilipokelewa na kati ya hizo, **Shilingi bilioni 2.905** ni fedha za matumizi mengineyo na **Shilingi bilioni 13.747** ni fedha za mishahara. Vilevile, **Shilingi bilioni 343.486** sawa na asilimia 51 ya fedha za maendeleo zilipokelewa.

## 4. Utekelezaji wa Miradi kwa mwaka 2018/2019

Katika mwaka 2018/2019, wizara iliendelea na utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali zinazolenga kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji; ufuatiliaji wa ubora wa maji; na kuboresha upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika maeneo ya vijijini na mijini; na kutekeleza masuala mtambuka.

Katika kipindi cha bajeti ya mwaka 2018/2019, jumla ya miradi **198** yenye vituo vya kuchotea maji **4,719** imekamilika na inawanufaisha wananchi wapatao **1,252,731** waishio vijijini. Aidha, miradi **653** inaendelea kutekelezwa katika halmashauri mbalimbali hapa nchini. Baadhi ya miradi ya kielelezo ya usambazaji wa majisafi na salama na usafi wa mazingira iliyotekelezwa vijijini na mijini ni kama ifuatavyo:

| Jina la Mradi | Maelezo kuhusu mradi | Hatua iliyofikiwa | |
|---|---|---|---|
| | | *2017/2018* | *2018/2019* |
| 1. **Mradi wa Same-Mwanga-Korogwe** | Mradi utatumia maji kutoka Bwawa la Nyumba ya Mungu na utahudumia miji ya Same na Mwanga pamoja na vijiji 38 vilivyopo kandokando ya bomba kuu katika wilaya za Same, Mwanga na Korogwe. Mradi utahudumia jumla ya watu **264,793** katika wilaya hizo. Ujenzi wa mradi umegawanyika katika vipande vinne. Kipande cha tatu bado kinatafutiwa fedha. | Ujenzi wa kipande cha kwanza - **asilimia 68**<br>Ujenzi wa kipande cha nne - **asilimia 37**<br>Ujenzi wa kipande cha tatu ulikuwa haujaanza | Ujenzi wa kipande cha kwanza- **asilimia 79**<br>Ujenzi wa Kipande cha nne - **asilimia 55**<br>Ujenzi wa kipande cha tatu umefikia - **asilimia 15** |
| 2. **Mradi wa Maji wa Vijiji 100 Vilivyopo Kando ya Bomba Kuu la KASHWASA** | Mradi wa maji wa vijiji 100 vilivyopo kandokando ya bomba kuu la maji kutoka Ziwa Victoria hadi miji ya Kahama na Shinyanga kwa kutumia maji ya Ziwa Victoria. Awamu ya kwanza ya mradi inahusisha vijiji 40. | Usanifu katika vijiji 33 ulifanyika na ujenzi wa mradi katika vijiji 14 ulikamilika na wananchi **38,348** wamenufaika | Ujenzi umeendelea katika vijiji saba na umefikia katika **asilimia 40** na **90**. |
| 3. **Mradi wa Maji katika Miji ya Tabora, Nzega, Igunga na Halmashauri ya Uyui** | Mradi wa kutoa maji kutoka bomba kuu la *KASHWASA* kupeleka katika Miji ya Tabora, Igunga, Nzega na Wilaya ya Uyui. Utakapokamilika, mradi utafikisha maji katika miji tajwa kwa asilimia 100 na kunufaisha wananchi wa vijiji wanaopitiwa na bomba kuu pamoja na vijiji vilivyopo katika halmashauri ya wilaya ya Uyui. | **Asilimia 15** | **Asilimia 68.5** |
| 4. **Mradi wa Maji katika Jiji la Mwanza na Miji ya Lamadi, Magu na Misungwi** | Mradi wa uboreshaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Jiji la Mwanza na Miji ya Magu, Misungwi na Lamadi. Mradi utanufaisha watu **197,844** katika maeneo yaliyotajwa. | **Asilimia 15** kwa Jiji la Mwanza na **asilimia 10** katika Miji ya Magu, Misungwi na Lamadi. | **Asilimia 75** kwa Jiji la Mwanza na **asilimia 87** katika Miji ya Magu, Misungwi na Lamadi. |
| 5. **Mradi wa Maji katika Jiji la Arusha** | Mradi wa majisafi ya kunywa na usafi wa mazingira Jijini Arusha unaotarajiwa kuongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 40 kwa siku hadi lita milioni 200 kwa siku na kuwezesha upatikanaji wa maji katika Jiji hilo kwa asilimia 100. | Sehemu kubwa ya mradi ilikuwa katika hatua za manunuzi na utekelezaji ulikuwa **asilimia 3.** | Ujenzi wa mradi umeanza na sasa umefikia **asilimia 30** |
| *6.* **Mradi wa Maji katika Mji wa Longido** | Mradi wa maji katika Mji wa Longido unalenga kuboresha huduma ya maji katika mji huo pamoja na kijiji cha Engi-karet.<br>Kukamilika kwa mradi wa Longido kumewezesha wananchi wapatao **16,712** wa Longido Mjini na wananchi wapatao **1,294** wa kijiji cha Engi-karet kupata huduma ya majisafi na salama. | Ujenzi wa kipande cha 1, 2 na 3 ulikuwa umefikia **asilimia 42** na ujenzi wa kipande cha nne ulikuwa umefikia **asimilia 75**. | Vipande vitatu vinavyohusisha ujenzi wa chanzo, ujenzi wa bomba kuu la kusafirishaji maji na ujenzi wa matanki umekamilika. Ujenzi wa kipande cha nne unaohusisha ujenzi wa kituo cha kusukuma maji umefikia **asilimia 95** |

| Jina la Mradi | Maelezo kuhusu mradi | Hatua iliyofikiwa | |
|---|---|---|---|
| | | *2017/2018* | *2018/2019* |
| ***7.*** **Mradi wa Ukarabati na Upanuzi wa Mfumo wa Kusambaza Maji katika Jiji la Dar es Salaam** | Mradi wa kukarabati na kusambaza majisafi katika maeneo ya Tegeta hadi Mpiji; Mpiji hadi Bagamoyo na Mbezi hadi Kiluvya. Kazi zinahusisha ulazaji wa mabomba (**KM 511.6**), ujenzi wa tanki la kuhifadhi maji (**lita milioni 5 kwa siku**) katika eneo la Salasala na ujenzi wa matanki manne katika maeneo ya Changanyikeni, Wazo, Bunju na Bagamoyo. Kukamilika kwa mradi kutawanufaisha wananchi wa maeneo 23[1] ambayo kwa sasa hayapati maji Jijini Dar es Salaam. | Mradi ulikuwa umefikia **asilimia 81**. | Mradi umekamilika na sasa upo katika awamu ya pili ya mradi itakayohusisha usambazi wa maji na kuunganisha wateja **64,000** katika maeneo tajwa. Hadi mwezi Aprili, 2019 mkandarasi amekamilika na ujenzi utarajiwa kuanza mwezi wa Mei, 2019. |
| **8. Ujenzi wa Mradi wa Maji Katika Mji Mpya wa Serikali – Mtumba, jijini Dodoma** | Mradi wa maji wenye kulenga kusambaza maji katika Mji mpya wa Serikali katika eneo la Mtumba, jijini Dodoma. Mradi umegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni kujenga tanki na miundo mbinu ya usambazaji maji (awamu ya kwanza) na kuunganisha maji katika ofisi mbalimbali (awamu ya pili) | Mradi ulikuwa katika hatua ya manunuzi | Sehemu ya kwanza imekamilika na sehemu ya pili imefikia **asilimia 80**. |

[1] *Maeneo haya ni: Mji wa Bagamoyo, EPZ Bagamoyo, Mpiji, Bunju, Mabwepande, Boko, Mbweni, Tegeta, Ununio, Wazo, Salasala, Kinzudi, Matosa, Mbezi Juu, Goba, Changanyikeni, Makongo, Kiluvya, Kibamba, Mbezi, Msakuzi, Makabe, Malamba Mawili na Msigani.*

## 5.Baadhi ya Miradi Mipya itakayotekelezwa kuanzia Mwaka 2019/2020

Pamoja na miradi mingine, Wizara ya Maji imepanga kutekeleza miradi mipya mikubwa na ya kimkakati miwili. Miradi hii ni mradi wa maji katika miji 28 utakaogharamiwa kwa fedha za mkopo kutoka Serikali ya India kupitia Benki ya Exim ya India. Mradi huu utagharimu **Shilingi trilioni 1.2** na unatarajiwa kunufaisha wananchi zaidi ya milioni sita. Miji itakayonufaika na mradi huu ni: Muheza (Tanga), Wanging'ombe (Njombe), Makambako (Njombe), Kayanga (Kagera), Makonde (Mtwara), Njombe, HTM/Korogwe (Tanga), Manyoni (Singida),Nanyumbu (Mtwara),Sikonge (Tabora), Chunya (Mbeya), Kasulu (Kigoma), Kilwa Masoko (Lindi), Rujewa (Mbeya), Mugumu (Mara), Geita, Chato (Geita), Singida, Kiomboi (Singida), Mpanda (Katavi), Chemba (Dodoma), Mafinga (Iringa), Uramba na Kaliua (Tabora), Pangani (Tanga), Ifakara (Morogoro), Rorya/Tarime (Mara), na Chamwino (Dodoma).

Mradi mwingine ni mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabia nchi Simiyu (Simiyu Climate Resilience Project) utakaotekelezwa kwa fedha za msaada kutoka shirika la Green Climate Fund na Serikali ya Ujerumani kwa jumla ya **Euro milioni 127.7 (sawa na shilingi bilioni 330)**. Mradi huu utatekelezwa katika Miji ya Bariadi, Lagangabilili na Mwanhuzi kwa kutumia chanzo cha maji kutoka Ziwa Victoria na unatarajia kunufaisha wananchi zaidi ya laki tatu kupitia miradi ya maji safi na salama, usafi wa mazingira na kilimo cha umwagiliaji.

## 6. Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka 2019/2020

Waziri wa Maji Mhe. Profesa Makame Mbarawa (Mb) ameliomba Bunge kuidhinisha jumla ya **Shilingi 634,196,197,530** kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2019/2020. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi 23,726,309,000** ambapo **Shilingi 6,266,714,000** sawa na asilimia 24 ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi Mengineyo (OC) na Shilingi 17,459,555,000 sawa na asilimia 76 ni kwa ajili ya kulipa mishahara (PE) ya watumishi wa Wizara na Chuo cha Maji.

Aidha, Mhe. Mbarawa (Mb) ameliomba Bunge liidhinishe bajeti ya maendeleo ya **Shilingi 610,469,888,530** ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 349,449,000,000** sawa na asilimia 57 ni fedha za ndani na **Shilingi 261,020,888,530** sawa na asilimia 43 ni fedha za nje.

## 7. Hitimisho na Shukrani

Wizara ya Maji inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maji ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji nchini. Mafanikio makubwa yanaendelea kupatikana katika sekta hii katika maeneo ya uendelezaji na ulinzi wa raslimali za maji; usambazaji wa maji kwa matumizi mbalimbali na ubora wa maji. Kazi kubwa imefanyika katika maeneo yote haya. Hata hivyo, bado kubwa ipo mbeleni katika kuhakikisha kuwa wananchi walio wengi wanapata huduma ya maji safi na salama ya kunywa na matumizi mengine muhimu.

Changamoto kubwa katika jitihada za Wizara ya Maji za kusambaza maji imekuwa ni kukosekana kwa uendelevu wa miradi ya maji vijijini. Changamoto hii inatarajiwa kutatuliwa kwa kiasi kikubwa na mfumo mpya wa uendeshaji wa sekta ya maji vijijini kupitia Wakala ya Maji Vijijini (RUWASA). Katika kukabiliana na changamoto mbalimbali katika sekta ya maji, tutaendelea kushirikiana na sekta binafsi pamoja na wadau mbalimbali wa maendeleo.

Kwa niaba ya Serikali, Waziri wa Maji, Mhe. Profesa Makame Mbarawa (Mb), anawashukuru sana wadau mbalimbali walioshirikiana na wanaoendelea kushirikiana na wizara katika utelekezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Wadau hawa ni pamoja na Serikali ya India kupitia Benki ya Exim ya India, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Ufaransa (AFD), Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW), Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya (EIB), Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (BADEA), Mfuko wa Maendeleo wa Nchi zinazozalisha Mafuta (OPEC Fund for International Development-OFID), Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait (Kuwait Fund),Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (SFD), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DFID), Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA), Shirika la Maendeleo la Ujerumani(GIZ), Global Environment Facility (GEF), Green Climate Fund, Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Shirika la Maendeleo la Ubelgiji (BTC), Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (UNDP) na Shirika la Misaada la Marekani (USAID). Aidha, Mheshimiwa Waziri anayashukuru Mashirika na Taasisi za Kidini na Taasisi zisizo za Kiserikali zinazoshiriki katika kuendeleza Sekta ya Maji.

Hotuba kamili ya Bajeti ya Waziri wa Maji inapatikana katika tovuti ya Wizara ya Maji yenye anwani: **www.maji.go.tz.**

# Nipashe Spoti




NYOTA WA5 WENYE NAFASI YA KUBEBA BALLON D'OR 2019 UK.16



## KITUU...

Straika wa Liverpool, Divock Origi (jezi namba 27) akiruka juu na kufunga bao la ushindi kwa timu yake katika mechi ya Ligi Kuu England dhidi ya Newcastle United iliyochezwa juzi usiku kwenye Uwanja wa St James' Park. Liverpool ilishinda mabao 3-2. **PICHA: MTANDAO**

## ISIKUPITE

Kocha wa zamani wa Manchester United, Jose Mourinho amepewa ofa ya mkataba wa miaka mitatu na klabu ya Roma, lakini Mreno huyo amewaeleza kuwa atakuwa tayari kujiunga na klabu hiyo endapo itafanikiwa kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.



# WACHEZAJI AMBAO WATAKUWA HURU EPL

**LONDON,** England

WAKATI msimu wa Ligi Kuu England ukikaribia kufikia mwisho, sasa tunaelekea kwenye kipindi cha majira ya joto ambapo dirisha kubwa la usajili linafunguliwa.

**Hapa wachezaji na mawakala wao wanakuwa katika kazi moja tu ya kutafuta malisho bora zaidi kwao.**

Na hii inaleta nafasi kwa klabu nyingine kusajili wachezaji wapya kwa ajili ya kuimarisha vikosi vyao.

Sasa hapa tunawaangalia wachezaji watano kwenye Ligi Kuu England maarufu EPL, ambao watakuwa huru wakati wa dirisha la usajili la kipindi cha majira ya joto. Na hapo watakuwa na uhuru wa kusajiliwa na timu yoyote waipendayo:

**5 GARY CAHILL - CHELSEA**

Nafasi yake kwenye kikosi cha kwanza haipo tena na mkataba wake utafikia mwisho wakati wa kipindi cha majira ya joto.

Kwa msimu huu karibu wote alikuwa akitumikia zaidi akiwa benchi. Tayari ameshastaafu soka la kimataifa na sasa ni wazi kwamba atakuwa na nafasi nyingine kwenda kutafuta malisho sehemu nyingine, kwani yupo huru kufanya makubaliano na klabu yoyote kwa sasa.

**4 OLIVIER GIROUD - CHELSEA**

Giroud alikuwa na msimu wa kuvutia msimu huu wa 2018-19 wakati alipokuwa kwenye kikosi cha mabingwa wa dunia, Ufaransa. Kwa sasa hana nafasi kwenye kikosi cha kwanza cha Chelsea huku akiwa ameanza mara moja tu tena kwenye mashindano ya Kombe la Ligi ya Europa.

Licha ya kuwa mshambuliaji hapo Chelsea mkataba wake unamalizika kipindi cha majira ya joto na ni wazi kwamba anaweza kurudi nchini Ufaransa kwa ajili ya kumalizia kipindi chake cha uchezaji.

**3 ANDER HERRERA - MANCHESTER UNITED**

Huu ni msimu wa tano wa Ander Herrera akiwa na Manchester United. Mchezaji huyu wa Hispania sasa muda wake unaonekana kuelekea ukingoni pale kwenye dimba la Old Trafford.

Uvumi umeenea kwamba amekubali mkataba wa miaka minne kutua kwa miamba wa Ufaransa, Paris Saint-Germain kwa mujibu wa BBC Sports. Halitakuwa jambo la kushangaza kumuona akiondoka kipindi cha majira ya joto kwani ndio atakuwa huru.

**2 VINCENT KOMPANY - MANCHESTER CITY**

Beki huyu wa kati wa kimataifa wa Ubelgiji amekuwa kiongozi mzuri zaidi kwenye vyumba vya kubadilishia nguo kwa kikosi cha Manchester City. Na sasa mkataba wake unafikia mwishoni baada ya kukaa hapo kwa kipindi cha miaka 10.

Majeruhi yamekuwa wakimsumbua zaidi kwa kipindi cha miaka kadhaa katika kipindi chake cha uchezaji, lakini anatumaini ataendelea kucheza sehemu nyingine, kwani ni wazi kwamba, Manchester City hawataweza kumwongeza mkataba mpya.


**1 JAMES MILNER - LIVERPOOL**

Baada ya kuondoka Manchester City kwenda Liverpool, James Milner amekuwa nguzo muhimu kwa mafanikio ya Liverpool inayonolewa na kocha Jurgen Klopp.

Amekua kiungo mzuri zaidi kwa Liverpool na pia kuna wakati amekuwa akicheza kama beki wa kushoto. Pamoja na uwezo wake huo, Jurgen Klopp ameonekana kupendelea kuwachezesha zaidi Fabinho na Naby Keita kwenye safu ya kiungo ya Liverpool.

Na hiyo ni wazi kuwa, Liverpool hawana mpango tena wa kumwongezea mkataba na hivyo atalazimika kuondoka akiwa mchezaji huru mwishoni mwa msimu huu.

**JE, WAJUA?**



MANCHESTER United imempa golikipa wake, David De Gea wiki moja ya kufanya uamuzi wa ama kubakia au kuondoka katika klabu hiyo. Mlinda mlango huyo raia wa Hispania anatarajia kumaliza mkataba wake mwakani na amepewa ofa ya kulipwa mshahara wa pauni 350,000 kwa wiki.

# MICHEZO

## NJE YA UWANJA

# United kumlipa Sanchez aondoke

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United inajiandaa kumlipa nusu ya mshahara wa mwezi, Alexis Sanchez kiasi cha pauni milioni 13 ili kuwezesha uhamisho wake katika kipindi cha majira ya joto.


Uamuzi wa mwisho wa mshambuliaji huyo wa Chile unabakia kuwa mikononi mwa kocha, Ole Gunnar Solskjaer, lakini United ipo tayari kumuachia mshambuliaji huyo.

Maofisa wa United wanajua kuwa mshahara wa Sanchez wa pauni 500,000 kwa wiki pamoja na bonasi utakuwa kizuizi kwa nyota huyo kupata klabu nyingine haraka.

Hivyo inaeleweka kwamba, sasa wanataka kumlipa asilimia 50 ya mshahara wake nyota huyo wa zamani wa Arsenal kama klabu nyingine itakuwa tayari kumsajili katika dirisha la usajili linalotarajiwa kufunguliwa hivi karibuni.

United inataka kumuuza Sanchez kwenda klabu nyingine baada ya nyota huyo kushindwa kung'ara tangu atue hapo kwenye dimba la Old Trafford.

Sanchez tangu alipowasili Old Trafford, ameshindwa kuonyesha kiwango kizuri kama ilivyotarajiwa na alivyokuwa kwenye timu yake ya zamani.







# NJIA AZAM ILIVYOTINGA FAINALI FA

Wachezaji wa Azam wakimpongeza straika, Donald Ngoma (jezi namba 11) baada ya kufunga bao pekee katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la FA iliyochezwa Ijumaa kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

**Na Adam Fungamwango**

GOLI la dakika ya 73 lililowekwa wavuni na mchezaji wa zamani wa Yanga, Donald Ngoma, liliiwezesha Azam FC kutinga hatua ya fainali ya mashindano ya Kombe la FA kwa mara ya pili kwenye historia ya klabu hiyo siku ya Ijumaa.

**Azam ilipata nafasi hiyo kwa kuichapa KMC FC, timu inayomilikiwa na Manispaa ya Kinondoni Dar es Salaam bao 1-0, katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, ulioko Chamazi jijini.**

Bingwa wa Kombe la FA ndiye huiwakilisha Tanzania Bara katika michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Kwa matokeo hayo, Azam ambayo kwa sasa imeshasalimu amri kwenye kinyang'anyiro cha kusaka ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, itapambana na mshindi wa mechi kati ya Lipuli dhidi ya Yanga inayotarajiwa kuchezwa leo kwenye Uwanja wa CCM, Samora mjini Iringa.

Mara ya mwisho kwa Azam kufika hatua hiyo ilikuwa ni msimu wa 2015/16 ilipocheza fainali dhidi ya Yanga na kuchapwa mabao 3-1 yaliyopatikana kwa mikwaju ya penalti baada ya timu hizo kutoka suluhu ndani ya dakika 90 za kawaida.

Kwa maana hiyo ni kwamba Azam haijawahi kutwaa Kombe la FA na kama ikifanikiwa kufanya hivyo msimu huu ambapo fainali inatarajiwa kuchezwa kwenye Uwanja wa Ilulu, Lindi itakuwa ni mara yao ya kwanza.

Ikumbukwe kuwa michuano hiyo mara ya mwisho ilichezwa mwaka 2002, kabla ya kusimama, na hatimaye Shirikisho la Soka Nchini (TFF) iliirudisha tena michuano hiyo ili bingwa wake ashiriki michuano ya kimataifa, Kombe la Shirikisho msimu wa 2015/16 ambayo Yanga ilikuwa bingwa kwa kuichapa Azam.

Msimu uliofuata 2016/17 Simba ilitwaa kombe hilo kwa kuifunga Mbao FC mabao 2-1 katika mechi ya fainali iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma na msimu uliopita 2017/18, Mtibwa Sugar ilifanikiwa kutwaa kombe hilo baada ya kuifunga Singida United mabao 3-2, mchezo ukipigwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid Arusha.

Azam FC haikufika fainali hiyo kirahisi, bali ilibidi ivuke mabonde na milima. Na hii ndiyo safari yao hadi kufika hapo.

**AZAM FC 2-0 PAMBA FC**

Ilianza kwenye raundi ya nne ya michuano hiyo iliyochezwa Januari 28 mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex ambapo ilifanikiwa kuichapa timu kongwe ya Pamba ya Mwanza mabao 2-0.

Mabao yote mawili kwenye mechi hiyo yalifungwa na winga wa zamani wa Simba, Ramadhani Singano 'Messi' dakika ya 18 na 53. Ushindi huo uliifanya Azam FC kutinga hatua ya 16 bora ya michuano hiyo.

**AZAM FC 3-0 RHINO RANGERS**

Azam ilifanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Kombe la FA kwenye pambano lililochezwa Februari 25 mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, mwenyeji wakiifunga timu ya Rhino Rangers ya Tabora mabao 3-0.

Mzimbabwe Tafazwa Kutinyu alianza kuipatia Azam bao katika dakika ya 21, na mabao mengine yalitinga kipindi cha pili dakika ya 58 yakifungwa na Salum Aboubakar 'Sure Boys" na Obrey Chirwa akifunga bao la tatu dakika ya 69.

**AZAM FC 1-0 KAGERA SUGAR**

Kiungo Joseph Mahundi alifanikiwa kuipeleka Azam FC hatua ya nusu fainali Machi 29 mwaka huu alipofunga bao pekee kwenye mechi ya robo fainali ya michuano hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.

Mchezaji huyo alifunga bao hilo dakika ya 80, huku golikipa wake tegemeo, Razak Abarola, akionyeshwa kadi nyekundu dakika ya 68 baada ya kumchezea vibaya mchezaji wa Kagera Sugar.

## Extra Time



MESSI



PIQUE



MBAPPE



VAN DIJK

# NYOTA WA5 WENYE NAFASI YA KUBEBA BALLON D'OR 2019



RONALDO

**BARCELONA,** Hispania

TUNAINGIA kwenye wiki ya mwisho ya kumalizika kwa msimu wa mwaka 2018/19 wa ligi mbalimbali barani Ulaya huku mabingwa wa Hispania, Italia na Ufaransa tayari wameshatambulika.

**Kwa sasa mbio za ubingwa huo zimebaki kwa nchi za England na Ujerumani kuwania taji la Ligi Kuu.**

Linapokuja suala la tuzo ya Ballon d'Or, Lionel Messi na Cristiano Ronaldo wametawala tuzo hiyo kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita, huku kila mmoja akishinda mara tano. Hakuna mchezaji mwingine aliyeshinda tuzo ya Ballon d'Or mara nyingi zaidi kuliko mchezaji mwingine yoyote katika zama ya soka la kisasa.

Tuzo hii imekuwa muhimu zaidi kwa wachezaji wa Ulaya kwenye kutambua vipaji vyao. Wachezaji kutoka Manchester City, Barcelona, Juventus, PSG na Liverpool wapo kwenye mbio za kuwania tuzo hiyo. Kwa mshangao mabeki wengi wamekuwa wenye orodha ya tuzo hii mwaka huu.

Hapa tunawaangalia wachezaji watano ambao wana nafasi ya kutwaa Ballon d'Or msimu huu.

### 5 GERARD PIQUE (BARCELONA FC)

Beki huyu wa kati wa Barcelona amekuwa nguzo ya mafanikio ya miamba hao wa Katalunya msimu huu. Wakati mchango mkubwa zaidi kwenye mafanikio ya kikosi hicho cha kocha, Ernesto Valverde ukitoka kwa Messi, lakini huwezi kuubeza mchango wa Gerard Pique.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 alishutumiwa kwa kutokuwa na kasi anapokuwa dimbani, lakini msimu huu amekuwa tofauti kabisa. Amesimama kwa kikosi cha Barcelona kama beki imara zaidi kwa kikosi hicho.

Mechi nyingi dhidi ya wapinzani wao wa soka la Hispania, Real Madrid, robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Manchester United, na ushindi dhidi ya Lyon ni baadhi ya mechi ambazo Pique alionyesha thamani yake kwa Valverde.

Amesifiwa zaidi na vyombo vya habari pamoja na mashabiki kutokana na kiwango chake msimu huu. Kama ataiongoza timu yake kutwaa mataji matatu msimu huu, ana nafasi ya kumaliza kwenye tatu bora na hatimaye kushinda tuzo.

### 4 CRISTIANO RONALDO (JUVENTUS)

Nyota huyu wa Ureno haitakuwa mara yake ya kwanza kushinda tuzo hiyo. Cristiano Ronaldo ameshinda tuzo hiyo mara tano na amemaliza akiwa kwenye tatu bora katika misimu nane mfululizo.

Mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or aliondoka kutoka La Liga kwenda Serie A kipindi cha majira ya joto na ameiongoza Juventus kutwaa taji la ligi msimu huu, lakini alishindwa kuivusha kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Nyota huyo wa zamani wa Real Madrid amefunga mabao 20 kwenye Ligi na kutoa pasi za mwisho 11 kwa wachezaji wenzake. Pia amefunga mabao sita kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Licha ya kuwa na msimu mzuri wa 2018/19, nafasi ya Ronaldo kushinda tuzo hiyo msimu huu inaonekana kuwa finyu. Kushindwa kwake kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, kunamaanisha kwamba, nafasi ya Ronaldo kutwaa tuzo ya Ballon d'Or mwaka 2019 ni ndogo.

### 3 KYLIAN MBAPPE (PARIS SAINT-GERMAIN)

Tangu akiwa pale Monaco msimu wa 2016/17, Kylian Mbappe amekuwa kwenye kiwango bora na cha kuvutia zaidi. Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 20 amekuwa nyota muhimu kwa Paris Saint-Germain kwa kufunga mabao muhimu kwa kikosi hicho kwa misimu kadhaa.

Chipukizi huyo alikuwa na wakati mzuri wakati akiisaidia Ufaransa kubeba kombe la Dunia nchini Ufaransa mwaka 2018. Katika mechi 22 alizoanza kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, msimu huu, Kylian Mbappe amefunga mabao 30 na kutoa pasi za mwisho tisa. Pia amefunga mabao manne kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Licha ya kufunga mabao mengi, PSG ilitolewa na Manchester United kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 bora. Pia walifungwa na Rennes kwenye Kombe la Ufaransa, kwa sasa wana taji la Ligi Kuu tu.

### 2 VIRGIL VAN DIJK (LIVERPOOL)

Mabeki mara chache wanapata tuzo hii, lakini Van Dijk msimu huu unaonekana kuwa bora zaidi kwake. Tangu atue pale Liverpool, Virgil van Dijk amekuwa ndio ukuta kwa kocha, Jurgen Klopp.

Tayari ameshinda tuzo ya mchezaji bora wa mwaka wa Ligi Kuu England msimu huu.

Na pia amekuwa beki wa kwanza kushinda tuzo hiyo tangu John Terry mwaka 2005. Ameonyesha uongozi imara kwa kikosi chake kuwaongoza katika mashindano yote msimu huu.

Liverpool bado ipo katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England na Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya. Liverpool imeruhusu mabao 20 kwenye Ligi Kuu msimu huu, kitu ambacho kinaifanya kuwa timu yake beki bora barani Ulaya.

Kama ataweza kuiongoza Liverpool kutwaa taji la Ulaya, atakuwa na nafasi kubwa zaidi ya kushinda tuzo ya Ballon d'Or.

### 1 LIONEL MESSI (FC BARCELONA)

Huu ni msimu mwingine bora kabisa kwa mchezaji huyu wa kimataifa wa Argentina. Lionel Messi amekuwa ndiyo nguzo ya Barcelona kuelekea kutwaa mataji matatu msimu huu. Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 31 ameiongoza kwenye safu ya upachikaji mabao kwa miamba hao wa Katalunya.

Amebakiwa yeye kuwa ndio muongozaji wa kupachika mabao baada ya kuondoka kwa Neymar. Messi amefunga mabao 34 na kutoa pasi za mwisho 13 katika michezo 27 ya La Liga msimu huu na ana mabao 12 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.


Barcelona pia imeshatwaa taji la Ligi Kuu Hispania na ipo katika hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Pia wapo kwenye fainali ya Kombe la Copa del Rey ambapo watacheza na Valencia.

Messi ameshinda tuzo hiyo mara tano na kama ataiongoza timu yake kutwaa mataji matatu msimu huu, ana nafasi kubwa ya kushinda tuzo hiyo ya Ballon d'Or.

## Nukuu

"Nimepokea kwa mshtuko mkuwa taarifa za msiba wa mlezi wetu wa Serengeti Boys, Dk. Reginald Mengi, sote ni mashabiki kwa namna alivyojitolea katika mpira wa miguu kuanzia ngazi ya klabu mpaka katika Timu za Taifa. Hakika mchango wake bado ulikuwa unahitajika. Kwa niaba ya TFF, natoa pole kwa familia yake. Kampuni ya IPP, ndugu, jamaa, marafiki na wanafamilia ya mpira wa miguu," **alisema Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia.**

"Dk. Reginald Mengi ameacha pengo kwani alikuwa ni mtu wa kujitoa, ila hatupaswi kulaumu zaidi ya kushukuru na kumuomba Mungu, njia yetu ni moja hatuwezi kukwepa hilo, inauma ila tunapaswa tumuombee kwa Mungu ampunguzie na adhabu za kaburi, pia alikuwa ni mtu wa michezo na mshauri wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) pamoja na kuwa ndani ya kamati ya maandalizi ya timu ya Taifa ya Vijana ,nSerengeti Boys akiwa ni mlezi," **Jonas Mkude, kiungo wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara alisema.**



"Watanzania tumepata msiba mkubwa, alikuwa ni mtu ambaye anapenda kuona maendeleo ya mtu mmoja mmoja, taasisi au vikundi. Pumzika kwa amani Mzee Mengi. Pole za dhati kwa familia yake pendwa, ndugu, jamaa, marafiki na IPP Media poleni sana," **aliandika mshambuliaji wa KRC Genk ya Ubelgiji na nahodha wa Timu ya Soka ya Tanzania (Taifa Stars), Mbwana Samatta.**

# IDD SULEIMAN 'NADO'

## Kutoka Ndondo Cup hadi kuzitesa Simba na Yanga



**Na Adam Fungamwango**

SIMBA na Yanga zinapocheza na Mbeya City kwa sasa kuna mchezaji mmoja tu ambaye anaweza kupachika mpira ndani ya wavu.

**Labda ni kwa sababu ya dharau kwa timu ndogo, lakini timu za Simba na Yanga kama zingekuwa zinakaribia kukutana na timu hiyo yenye maskani yake jijini Mbeya, zingekuwa zinamuwekea mikakati mizito ya kumzuia mchezaji huyo.**

Si mwingine ni Idd Suleiman 'Nado'. Mchezaji huyo mwenye uwezo wa kucheza nafasi ya kiungo mshambuliaji na pia kama mshambuliaji wa kati au winga, amekuwa na bahati kubwa ya kuzifunga timu hizo kongwe tangu alipoanza kuichezea Mbeya City ambapo anamaliza msimu wa pili sasa.

Ijumaa iliyopita alifunga bao dakika 21 dhidi ya Simba, goli lililoonekana kama vile linakwenda kuwaweka katika nafasi ngumu katika mbio zake za kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya pili mfululizo kama si magoli ya Jonas Mkude na Meddie Kagere.

**KUFUNGA MAGOLI BILA TIMU KUSHINDA**

Nado amekuwa na bahati ya kufunga magoli katika mechi dhidi ya Simba na Yanga, lakini bahati mbaya kwake ni kwamba hata kama akifanya hivyo, timu yake ya Mbeya City bado imekuwa haiibuki na ushindi.

Aprili 22, 2018, katika msimu wa Ligi Kuu uliopita alifunga bao la kusawazisha dakika ya 90 kwenye Uwanja wa Sokoine dhidi ya Yanga na mechi ikaisha kwa sare ya bao 1-1.

Desemba 29 mwaka jana, mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu msimu huu, Nado aliifungia Mbeya City bao dakika ya 24 kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, huku Heritier Makambo akiifungia Yanga mabao mawili dakika ya 17 na 41, Yanga ikapata ushindi wa magoli 2-1.

Hali kama hiyo ilijitokeza Ijumaa iliyopita kwenye Uwanja wa Sokoine, mchezaji huyo alipofunga bao kwa kuwafungasha "tela" mabeki wa Simba kabla ya kuachia shuti kwa mguu wa kushoto uliojaa wavuni.

Ni mechi ambayo vile vile timu yake haikushinda zaidi ya kuchabangwa mabao 2-1.

Nado anaingia kwenye orodha ya wachezaji waliopata magoli kwenye mechi ambazo timu zao zilicheza na Simba na Yanga msimu huu.

Amefikisha magoli saba kwenye Ligi Kuu msimu huu, ukiwa ni msimu wake wa pili akiichezea Mbeya City.

**ALITOKEA NDONDO CUP**

Ni mchezaji ambaye alisajiliwa na Mbeya City mwaka 2017 akitokea mtaani kwenye michuano ya Ndondo Cup na kuanza kucheza Ligi Kuu msimu wa 2017/18.

Kwenye michuano na Ndondo Cup, alikuwa akiichezea timu ya Manzese United ambapo aliiwezesha timu hiyo kutwaa kombe hilo, lakini ni mmoja wa wachezaji ambao waliwavutia makocha wengi, hatimaye kupelekwa Mbeya.

**AMEANZA KUWINDWA**

Tayari klabu kadhaa zimeshaanza 'kummezea mate' kutaka kumsajili katika dirisha la usajili la msimu ujao litakapofunguliwa.

Klabu kubwa za soka hapa nchini ambazo ni Simba, Yanga na Azam FC zimeshaanza kupigana kumbo kutaka saini ya nyota huyo.

Na huenda moja ya klabu hizo zikampata kiulaini kutokana na kumaliza mkataba wake msimu huu.

Uwezo wake wa kufunga magoli, upambanaji, pamoja na kuonekana ana uwezo na si mchezaji wa kukamia mechi moja, au wa msimu mmoja, kwani kiwango chake alichotoka nacho Ndondo Cup bado ameendelea kuwa nacho na kukilinda.

**NAJUA WAJUA**



TIMU ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), itacheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Misri ifikapo Juni 12, jijini Cairo, ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya Fainali za Kombe la Afrika (AFCON 2019) ambazo zitachezwa kuanzia Juni 21 hadi Julai 13 mwaka huu. Mara ya mwisho Stars kushiriki fainali hizo ilikuwa mwaka 1980.

# UNITED INAPASWA KUSAJILI HAWA WA5




JADON SANCHO

**MANCHESTER,** England

WAKATI wa kuanza kwa msimu wa 2018/19, Manchester United ilimsajili beki wa kulia wa Ureno, Diogo Dalot kutoka Klabu ya Porto na kiungo wa kumsaidia Paul Pogba, Fred kutoka Shakhtar Donetsk.

**Hata hivyo, hitaji la Mourinho la beki wa kati halikukamilishwa na alianza msimu akiwa na Lindelof, Bailly, Smalling, Jones na Rojo kama ndio mabeki wao.**

Bila ya shaka yoyote, Manchester United imekuwa na wakati mgumu zaidi kupata beki imara huku Eric Bailly akiwa na kiwango kinachapanda na kushuka wakati Jones, Smalling au Rojo wakishindwa kufikia matarajio na Lindelof ameshindwa kuonyesha kiwango cha juu.

Huku wachezaji kama Ander Herrera na Juan Mata wakitarajia kuondoka kama wachezaji huru kipindi cha majira ya joto, Ole sasa anakabiliwa na mtihani wa kukitengeneza kikosi na hapa tunaangalia wachezaji watano ambao anatakiwa kuwasajili.

**5. AARON WAN-BISSAKA**

Aaron Wan-Bissaka amekuwa na kipindi kizuri msimu huu pale Crystal Palace, akicheza kwa kujituma kwenye nafasi ya beki wa kulia.

Mchezaji huyu wa kimataifa wa England chini ya umri wa miaka 21 ameweza kukaba mara 149 msimu huu na kumfanya kuwa na asilimia 68% ya ukabaji mzuri zaidi kwa mchezaji kijana.

Ameokoa hatari 147 na kuwa mmoja wa mabeki bora wa pembeni vijana msimu huu. Kama United watampata mchezaji huyu, itakuwa salama kwao kuweza kuimarisha kikosi chao kwenye safu ya ulinzi.

**4. ADRIEN RABIOT**

Adrien Rabiot anapanga kuondoka Paris Saint Germain akiwa mchezaji huru kipindi cha majira ya joto, baada ya kushindwa kufikia makubaliano kati yake na klabu. Yeye mwenyewe akiwa amebainisha kwamba anataka kwenda Barcelona, inaonekana wazi kuwa anaweza asiwe na nafasi baada ya kusajiliwa kwa Frenkie de Jong Januari.

Huku Ander Herrera akiwa anatarajiwa kuondoka klabuni hapo kipindi cha majira ya joto kwenda PSG, itakuwa kazi rahisi kwa Manchestet United kumpata kirahisi Rabiot akiwa mchezaji huru.

Rabiot kiuchezaji ni bora zaidi ya Herrera wakati linapokuja suala la ubunifu na uwezo binafsi dimbani. Rabiot ana kipaji kizuri na anaweza kuwa msaada mkubwa zaidi kwa United kuliko hata Herrera.

Huku mfumo wa mishahara wa United una uwezo wa kufikia kile anachokitaka Rabiot, hivyo wana nafasi nzuri zaidi ya kuweza kumsajili.

**3. WILFRED NDIDI**

Nyota Wilfred Ndidi amekuwa mchezaji wa aina yake pale Leicester City msimu huu na ameisaidia zaidi timu yake kuliko mchezaji mwingine yoyote kwenye kikosi cha timu hiyo.

Huku Leicester ikiwa imejengwa na kikosi chenye vijana kama vile Maddison, Tielemans na Ndidi, ni wazi kwamba United italazimika kutumia kiasi kikubwa cha fedha ili kumpata mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal.

Akiwa ndio kwanza ana umri wa miaka 22, inaweza kuwagharimu United kiasi cha pauni milioni 50. Na kwa kuwa kiwango cha sasa cha Nemanja Matic kimeshuka ni wakati sasa wa United kumsajili Ndidi ili kuimarisha kikosi chake.

**2. JADON SANCHO**

Chipukizi huyu ambaye aliondoka Manchester City kwenda Dortmund akitafuta nafasi ya kucheza mara kwa mara inaonyesha wazi kwamba Manchester City na Pep walipoteza kipaji cha ukweli. Amekuwa na msimu wa kuvutia pale Borussia Dortmund, akisaidiana na Marco Reus na Paco Alcacer.

Amefunga mabao 11 na kutoa pasi za mwisho 14 msimu huu kwenye Bundesliga, na amekuwa na upatina mzuri na Reus kwenye safu ya ushambuliaji.

Sancho ndio kwanza ana umri wa miaka 19 na itakuwa vigumu mno kuondoka nchini Ujerumani. Pia ukiacha ukweli kwamba ni mchezaji wa zamani wa City, United itakuwa na wakati mgumu kumchukua nyota huyo, ingawa anaweza kuwa msaada mkubwa zaidi kwao.

**1. KALIDOU KOULIBALY**

Safu ya ulinzi ya Napoli imekuwa imara zaidi huku ikilindwa na Koulibaly na kuifanya kuwa na ukuta usiopitika msimu huu.

Huku United ikiwa na tatizo kubwa la beki wa kati, ni wazi kwamba Koulibaly atakuwa suluhisho la matatizo ya ulinzi ya klabu hiyo endapo itafanikiwa kumnasa.

Ingawa inaweza kuwagharimu United ada itakayoweka rekodi ya dunia, lakini hawatakuwa na namna nyingine ya kuacha kumsajili beki huyo. Ujio wa beki huyo kwa mashetani wekundu kutaifanya safu yao kuepukana na matatizo ambayo Jose Mourinho alikuwa akiyapigia kelele kwa kipindi kirefu.

**NDANI YA 18**



MSHAMBULIAJI Mtanzania Mbwana Samatta, juzi alifikisha mabao 62 akiwa na kikosi cha Genk ya Ubelgiji akiwa ameichezea mechi 153 za mashindano yote tangu alipojiunga na timu hiyo Januari mwaka 2016 akitokea TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

Nipashe
Spotika




TUNAINGIA kwenye wiki ya mwisho ya kumalizika kwa msimu wa mwaka 2018/19 wa ligi mbalimbali barani Ulaya huku mabingwa wa Hispania, Italia na Ufaransa tayari wameshatambulika.

Uk. 16-17




# HAPA NDIPO FERGUSON ALIPOWEKA ALAMA ISIYOFUTIKA

**MANCHESTER,** England

SIR Alex Ferguson ni mtu mwenye heshima kubwa sana katika klabu ya Manchester United.

Alifanikiwa kutengeneza dunia ya peke yake pale Manchester United. Dunia ambayo ilivutia watu wengi kuja kuishi kwa furaha kubwa.

Anakumbuka nyakati ambazo alichukua Manchester United. Zilikuwa nyakati ngumu ambazo Manchester United walikuwa wanapitia.

Hilo lilikuwa linaonekana kwa macho ya mbele kabisa bila uficho. Ndizo nyakati ambazo Liverpool walikuwa wamejitengenezea ufalme wao wa peke yao. Hakuna ambaye alikuwa ana uwezo wa kugusa falme yao. Ilikuwa falme imara sana kuzidi falme zote kwenye ardhi ile ya malkia.

Ilikuwa falme ambayo ilitawala kwa muda mrefu. Na hakukuwapo na mtu wa kukohoa mbele ya Liverpool kwa kipindi hicho.

Miaka 19 timu nyingi zilikuwa katika utumwa wa ufalme wa Liverpool. Iliburuza kila kitu ambacho iliona inastahili kuburuza. Ilisimama mbele na kujitanua na wengine wakipiga goti chini na kushuhudia mbele yake. Haya ndiyo yalikuwa maisha halisi ya Liverpool.

Maisha ambayo hata kwenda bafuni walitumia maziwa kuogea. Hawakuwa na wasiwasi kabisa. Ila walikuwa wanaishi maisha ambayo walistahili kuishi kipindi hicho.

Utawaambia nini kuhusu neno njaa wakusikie kwa kipindi hicho? Utahubiri nini Kwao hakukuwepo na jua la ukame, kila uchwao walikuwa wanapata mvua ya maziwa tu. Mito, bahari na maziwa yote yaliyokuwapo katika kiunga chao yalitapakaa kimiminika hiki.

Hii ndiyo ilikuwa Liverpool, Liverpool yenye miraba minne. Liverpool yenye shibe tele. Liverpool ambayo chozi kwao lilikuwa nadra kushuka.

Wakati unaizungumzia shibe ya Liverpool, basi kulikuwapo na njaa kubwa sana kwa Manchester United.

Hapa hadithi zote zilizohusu furaha walikuwa wanazisikia kwa Liverpool pekee. Mahasimu wakubwa sana.

Ilikuwa inawauma sana. Adui yako kunenepa afu wewe unakonda ni maumivu makubwa sana. Maumivu ambayo walikuwa wanayapitia sana Manchester United. Walisimangwa sana kipindi hicho. Hawakuwa na uwezo wa kujitanua barabarani kwa kujitapa kuhusiana na neno mafanikio mpaka pale Alex Ferguson alipokuja Manchester United.

Mtu ambaye kwa baadaye jina lake liliongezeka kutoka Alex Ferguson na kuwa Sir. Alex Ferguson baada ya kupata mafanikio makubwa mwaka 1999 kwa kuchukua vikombe vitatu.

Mtu ambaye aliikuta United ikiwa klabu ya tatu kwa kuchukua vikombe vingi vya Ligi Kuu England nyuma ya Liverpool na Arsenal.

Mtu ambaye hakutazamiwa sana kufanya makubwa akiwa na wanajeshi hawa wenye kutumia magwanda ya rangi nyekundu kwenye vita. Nani alitegemea Ferguson atakuwa mfalme mkubwa wa soka la England? Mtu ambaye alitoka kwenye timu ambayo haikuwa na jina.

Mtu ambaye alikuwa hajawahi hata siku moja kuiongoza timu kubwa kwenye maisha yake ya ukocha. Lakini akapewa jukumu la kupambana na Liverpool ya moto. Lakini alifanya tofauti na matazamio ya watu wengi. Alirudisha furaha kubwa ndani ya Manchester United.

Huyu ndiye aliyeleta kiangazi kikubwa kwenye ufalme wa Liverpool na kuleta masika kila mwaka katika kikosi cha Manchester United.

Alishinda kila kikombe ambacho kilikuwa kinashindaniwa na kikosi cha United katika maisha yake ya ukocha.

Hatimaye akaanza kurudisha furaha iliyokuwa imepotea kwenye kikosi cha Manchester United kwa muda mrefu wa soka.

Akawa mtawala rasmi wa soka la England. Aliogopeka mno. Alikuwa na uwezo wa kushinda kombe lolote akiwa na aina yoyote katika kikosi alichokuwa nacho. Alikuwa na uwezo wa kuwafanya wachezaji ambao kwenye macho ya kawaida ya watu walikuwa wakubwa na wakaonekana wawe na timu hatari.

Hakuamini katika ukawaida wa mchezaji mmoja mmoja. Wala hakuamini katika uhatari wa mchezaji mmoja mmoja. Kwake yeye aliamini katika uhatari wa timu kwa ujumla. Ndiyo maana alikuwa na uwezo mkubwa sana wa kujenga timu imara kupitia wachezaji ambao walikuwa wanaonekana wa kawaida.

Wachezaji ambao hakuwa na ukawaida usio wa kawaida. Wachezaji ambao walikuwa na uwezo wa kupigana sana kwa ajili ya jezi ya Manchester United.

Ndiyo maana hata muda wa yeye kuondoka Manchester United ulipowadia kitu cha kwanza kukiona baada ya kutakiwa kutoa maoni ya mrithi wake ni kupata kocha wa aina yake.

Kocha ambaye alikuwa na uwezo wa kutumia wachezaji wa kawaida kutengeneza timu hatari.

Hapa ndipo kosa kubwa ambalo lilifanyika ambalo mpaka Leo linaigharimu Manchester United kwenye mafanikio yao. Walimleta David Moyes, walisahau soka la sasa limebadilika. Lilikuwa linahitaji wachezaji hatari na kocha hatari.

Na kocha ambaye alistahili kuwa mrithi wa Sir Alex Ferguson alikuwa anastahili kuwa kocha hatari ili kuendeleza utamaduni wa ushindi wa klabu hiyo.

Lakini ikawa tofauti, Sir Alex Ferguson akafanya kosa mwishoni kosa ambalo linawahangaisha hadi sasa kwa kukifuta kivuli chake cha mafanikio.

## USILOLIJUA

TOTTENHAM imeungana na Borussia Dortmund pamoja na Bayern Munich katika mbio za kuwania saini ya kiungo wa Ajax na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Donny van de Beek ambaye ana umri wa miaka 22.



# Tanesco yaomba umma udhibiti huduma

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

SHIRIKA la Umeme Tanzania (Tanesco) katika Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, limewaomba wateja wake kutoa taarifa pindi wanapoona shughuli za kibinadamu zinafanyiwa ikiwamo uchomaji moto jirani na miundombinu ya umeme ili kuepusha athari zinazoweza kutokea ikiwamo vifo.

Hayo yalisemwa na Mhandisi Ibrahim Kiungu, kwenye Kikao cha Baraza la Mamlaka ya Mji mdogo wa Rujewa, ambapo aliwaomba madiwani kusaidia kutoa elimu itakayosaidia wananchi kuacha tabia ya kufanya shughuli zao karibu na maeneo yenye miundombinu ya umeme.

Mhandisi Kiungu alisema wananchi wamekuwa wabishi kufuata maelekezo ya Shirika, yanavyotaka kuacha kufanya shughuli za kibinadamu karibu na miundombinu ya umeme na kwamba majanga yanapotokea hutupiwa lawama.

Alisema kwa kuwa Madiwani ndio wenye watu, wasaidie kutoa elimu ya kutambua athari za kufanya shughuli karibu na miundombinu ya umeme, lakini pia kukabiliana na majanga ya mlipuko wa umeme yanapotokea.

"Mara kwa mara shirika letu limekuwa likitupiwa lawama kwa madai ya kuhusika na milipuko inayotokea kwenye umeme, wanasahau kuwa wananchi ndio wanasababisha kwa sababu wanafanya shughuli zao karibu na miundombinu hiyo... tunaomba tuache kulalamika, tufuate maelekezo," alisema Mhandisi Kiungu.

Aidha, Kiungu aliwahakikishia wakazi wa Mbarali kuwa Shirika linaendelea na jitihada za kuhakikisha wateja wake wanapata umeme wa uhakika.

Alisema Serikali inaendelea na jitihada za kuboresha miundombinu ya uzalishaji umeme kwenye vyanzo vya uzalishaji, na kwamba baada ya kukamilika kero ya kukatika kwa umeme itakuwa historia, aliwaomba wananchi kuilinda miundombinu ya umeme iliyopo ili wapate umeme.

Kiungu aliwaeleza wananchi kushuka kwa gharama za umeme kutoka Sh. 102,007 hadi Sh. 27,000 kwa mita 30 kutoka nguzo ilipo ya umeme, ni dhamira ya Serikali ya kuhakikisha wananchi wa kipato cha chini wananufaika na nishati hiyo.

Aidha katika Kikao hicho cha Baraza, Mwenyekiti, Chameta Godigodi, aliiomba Serikali iwapatie asilimia 100 ya ukusanyaji wa mapato ili fedha hizo zitumike katika shughuli za maendeleo kama zinavyofanya Mamlaka za miji mingine nchini.

Ofisa Mtendaji wa Mamlaka hiyo, Ntuntufye Chamba, aliwataka wenyeviti wa vitongoji na viongozi wengine kusimamia kikamilifu suala la uingizwaji wa mifugo katika mashamba ya mpunga kwa kuwa msimu wa kuvuna umekaribia.




Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali Nickodema Mwangela (aliyesimama), akiwa katika kikao kujadili ujirani mwema kuhusu kuhamahama kwa Mto Songwe ambao ni mpaka wa Tanzania na Malawi, wilayani Ileje. **PICHA: RAHIM YUNUS**

# Wachimbaji waomba usalama soko la madini

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

WACHIMBAJI na wafanyabiashara wa dhahabu katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, wameiomba Serikali kuwahakikishia usalama wa fedha na mali zao katika soko la madini lililofunguliwa mjini Chunya.

Wamedai sababu ni kuwa watumishi wa Idara ya Madini ni wachache ukilinganisha na changamoto za usalama wa wachimbaji.

Waliyasema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa soko la dhahabu uliofanywa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini, Prof. Simon Msanjila, ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Bosco Mwanginde, alisema miongoni mwa changamoto zao ni Usalama mdogo kwenye soko wakihofia vitendo vya uhalifu pamoja na upungufu wa watumishi na kusababisha kutopata huduma kwa wakati.

Mwanginde alisema wanaipongeza Serikali kwa kuweka soko la pamoja la madini ambalo litatoa nafasi kila mfanyabiashara wa dhahabu kuwa kwenye ushindani wa bidhaa yake, lakini bado wana wasiwasi kuhusu usalama wao.

"Tunaiomba serikali kuimarisha ulinzi na usalama kwenye eneo la soko letu la madini na migodini ili kufanya biashara hiyo kwa uhuru, usalama huo utawavutia wawekezaji wakubwa," alisema Mwanginde.

Prof. Msanjila alisema Serikali imejipanga kuhakikisha soko la madini linatatua changamoto kubwa zinazo wakabili wadau wa sekta ya madini.

Alisema kwa kuanzia Serikali imeanzisha soko la pamoja la madini ambalo linatoa fursa kuanzia mchimbaji mdogo mpaka mkubwa kuuza dhahabu yake sambamba na kuwatafutia wanunuzi.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Marryprisca Mahundi, aliwahakikisha wachimbaji wa dhahabu na wafanyabiashara kuwa wamejipanga kuhakikisha ulinzi na usalama maeneo ya sokoni na migoni umeimarishwa.

# Jamii yatahadharishwa mauaji ya wenye ualbino

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JAMII nchini imeshauriwa kuachana na imani potofu za kishirikina zinazodanganya kuwa viungo vya watu wenye ualbino ni dili na vinafaa kutajirisha watu, hali inayosababisha kuuawa na wengine kukatwa viungo.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Ofisa Ulaghabishi wa Shirika la Under The Same Sun (UTSS), Kondo Seif, akiwa mkoani hapa wakati wa kushiriki mbio za Tulia Marathon.

Seif alisema imani za kishirikina zimekuwa kichocheo kikubwa cha watu wenye ualbino kukatwa viungo vyao ili wengine wajitajirishe na kwamba imani hizo zimekuwa zikidanganya kwa kuwa kiungo cha binadamu hakiwezi kumtajirisha mtu.

"Nawasihi ndugu zangu achaneni na imani za kishirikina, watu wenye ualbino ni watu kama nyie kwa nini mnawaua. Hata mkiwaua hamfaidiki chochote, sote tumeumbwa na Mungu tuishi kwa amani na upendo," alisema Seif.

Seif alisema kwa kushirikiana na wadau wengine wamekuwa wakitoa elimu ya kupinga mauaji kwa watu wenye ualbino na imesaidia kwa sababu vitendo hivyo haviripotiwi mara kwa mara kama zamani.

Aliwashauri wananchi kila mmoja kuwa mlinzi wa mwenzake na kutoa ripoti kwenye vyombo vya usalama yanaporipotiwa matukio ya mauaji.

Katika kuhakikisha watoto wenye ualbino wanatimiza ndoto zao kupitia Elimu, Under The Same Sun linasomesha zaidi ya wanafunzi 400.

Wanafunzi hao wako katika ngazi mbalimbali kuanzia awali hadi shahada ya uzamivu na kwamba wapo wengine wameajiriwa, na kwamba hatua hiyo imesaidia watu hao kuwa mabalozi kwa watu wanaopanga kuwadhuru kwa kuona viungo vyao ni dili.





# WaTz watakiwa kuthamini elimu ya nchi yao

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Avemaria Semakafu, amewataka Watanzania kuacha tabia ya kuikosoa na kuidharau elimu inayotolewa nchini kwa madai kuwa haina ubora ikilinganishwa na mataifa mengine.

Dk. Semekafu aliyasema hayo jana jijini hapa wakati alipokuwa akitoa zawadi kwa washindi wa shindano la uandishi wa insha kwa ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (Sadec).

Alisema Watanzania wamekuwa wa kwanza kuizungumzia vibaya elimu inayotolewa nchini pamoja na walimu waliopo nchini kwa madai kuwa hawana ubora katika kufundisha ikilinganishwa na wa nchi nyingine.

"Tabia ya kuzidharau shule zetu za serikali kuwa hazifanyi vizuri si nzuri kwani walioongoza katika mashindano haya wengi wametoka katika shule zetu zinazoonekana hazifai na zile za kata na walimu wake walewale ambao watu wanawaita wa 'voda fasta'," alisema Dk. Semakafu.

Alisema Watanzania watakiwa kuwa mstari wa mbele kuipongeza serikali kwa kuwa elimu inayotolewa nchini ina ubora wa kutosha tofauti na maneno ya baadhi ya watu.

"Mimi mwenyewe nimesoma katika shule za serikali toka naanza masomo ya awali hadi PhD yangu kupitia shule zetu hizi hizi za serikali zinazo dharaulika, lakini pia hata walimu wangu walionifundisha wametoka katika shule za serikali," alisema.

Naye, Mratibu wa mashindano hayo, Sylvia Chinguwile, aliwapongeza walimu wa wanafunzi walioshiriki kwa usimamizi uliowawezesha kufikia mafanikio ya kupata ushindi katika mashindano.

"Natoa wito kwa walimu na wazazi kuzidi kuwahimiza wanafunzi kushiriki mashindano haya na mengine yatakayojitokeza kwa kuwa uzoefu umeonyesha washindi wa mashindano haya hufanya vizuri kwenye mitihani yao ya mwisho ya kitaaluma," alisema Chinguwile.

Mmoja wa wanafunzi walioshiriki mashindano hayo Inoccent Shirima, aliwaomba waandaaji hao kutumia lugha ya Kiswahili ili kuitambulisha nje ya mipaka ya Tanzania.

# 'Viongozi wa dini jiepusheni na siasa'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

VIONGOZI wa dini nchini, wametakiwa kuepuka kujiingiza kwenye masuala ya siasa kwa kuwa wanaweza kusababisha madhara makubwa.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, alipokuwa akifungua rasmi mkutano wa mahubiri ya Dodoma Net Event yenye kaulimbiu 'Uzoefu wa nguvu ya Mungu', katika Kanisa la Waadventista Wasabato Dodoma kati, jijini hapa.

Masauni alisema Watanzania wameshuhudia madhara makubwa yaliyotokea nchi zingine ulimwenguni kwasababu ya wanasiasa kutumia dini kutimiza matakwa yao ya kisiasa ni vyema wakajiepusha.

"Wanaamini kuwa kutumia dini wanaweza kuungwa mkono jambo ambalo ni hatari kwa mustakabali wa nchi, nchi yetu imejengwa kwa misingi mizuri, kuna wakati tumeshuhudia watu wakinyemelea kwa kutumia makanisa na misikiti kwa malengo ya kisiasa," alisema.

Alisema ni makosa makubwa kutumia dini kutekeleza matakwa binafsi ambayo yanasababisha kutenda mambo yasiyopaswa kwenye jamii.

"Kiongozi au muumini wa dhehebu la dini yoyote, ambaye hatatii sheria za nchi serikali haitasita kumchukulia hatua bila kujali nafasi yake, dini yake, atashtakiwa kwa kitendo chake cha kufanya kosa, viongozi wa dini na waumini waendelee kutii sheria za nchi," alisema.

Aidha, aliliomba kanisa hilo kuombea nchi na kufundisha maadili kwa taifa ili wale wachache wanaoendekeza imani za kishirikiana waachane nazo.

Akizungumzia rushwa, Masauni alisema bado ni tatizo licha ya serikali kuendelea kushughulikia na kuhimiza Watanzania kuondoa suala hilo kwenye mioyo yao ili liweze kuisha.

Alilitaka kanisa hilo kuwekeza kwenye miradi mikubwa itakayohudumia makao mkuu ya nchi kama vile shule, kumbi za mikutano na viwanda na serikali itahakikisha inatoa ushirikiano unaostahili.

"Naamini mikutano hii itakayorushwa nchi nzima itabariki Watanzania wote, na muendelee kuwa mstari wa mbele kudumisha amani na ushirikiano wa taifa letu, kanisa hili limeendelea kufuata misingi iliyoasisiwa na waasisi wa taifa letu," alisema.

Akitoa neno la shukrani, Mchungaji Dk. Godwin Lekundayo, alisema kuna maeneo machache vijana wanasumbuliwa kulazimishwa kusoma na kufanya kazi siku ya Sabato ambayo ni ya ibada.

"Tunakuahidi kama viongozi kuabudu bila kuvunja sheria, na hatupaswi kujihusisha na mambo ya siasa, tunatakiwa kuongea mambo ya dini, biblia inatosha haihitaji kujiingiza kwenye siasa, tunaahidi hatutajihusisha kwenye siasa, tuache siasa ibaki kwa wanasiasa tubaki sisi kuhubiri injili," alisema.

Alisema wataendelea kuhimiza kutokashifu dini nyingine na kuhubiri mambo ya dini zao.



Mkuu wa idara ya Mazingira jiji la Dodoma, Dickson Kimaro, akizungumza na wakazi wa Kata ya Kizota alipokuwa akiwahimiza umuhimu wa uwekaji wa vifaa vya kuhifadhia taka kwenye mitaa yao. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Miradi ya maji kuwasulubu wabunge 2020

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WABUNGE wameitaka serikali kutekeleza miradi ya maji kama ilivyopangwa ili kuwapunguzia maswali magumu wakati wa Uchaguzi Mkuu 2020.

Wakichangia bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2019/20, walisema fedha zilizotengwa kwenye miradi ya maji zitolewe ili ikatekelezwe na kuondoa maswali kwa wananchi wakati wa uchaguzi.

Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, alisema kama fedha zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ya Maji zitatolewa wabunge hawatatumia nguvu kubwa majukwaani.

"Ilani ya CCM inasema ifikapo mwaka 2020 tutakuwa tumefikia asilimia 85 ya miradi ya maji itakayotekelezwa, tusipowapa fedha za kutosha Wizara ya Maji tutakuwa na maswali magumu sana mwakani," alisema Chikota.

Alisema Uchaguzi Mkuu mwakani haupo mbali hivyo wizara ipewe fedha za kutosha ili wasipate kazi ya kuzungumza maneno marefu majukwaani.

Aidha, alisema baada ya Bunge kupitisha mabadiliko ya Sheria namba 5 ya inayotoa nafasi ya kuanzishwa Wakala wa Maji Vijijini (Ruwasa), wakati umefika sasa kwa serikali kufanya maandalizi ya kutosha ili itakapoanza kutekeleza majukumu yake ifanye kazi zake kwa ufanisi.

"Mamlaka ya serikali za mitaa zina hadhi tofauti, mhadisi wa maji ukimwambia atumie gari la halmashauri hatakuwa na gari kwasababu hakuwa na hilo gari, hivyo ni vema tukaanza maandalizi ya kutosha ili ikianza kazi basi tusijeilaumu," alisema.

Chikota, aliiomba wizara kutoa idhini ya utekelezaji wa mradi wa kutoa maji Mitema hadi Halmashauri ya Nanyamba ili meneja anayetekeleza mradi wa Makonde ajumuishe na kuwa sehemu ya mradi huo.

Alibainisha kwa sasa asilimia 45 ya wananchi wa Halmashauri ya Nanyamba ndio wanaopata maji na kwamba mradi huo ukitekelezwa, wananchi zaidi ya asilimia 85 watapata maji.

Mbunge wa Mpwapwa (CCM), George Lubeleje, alisema katika jimbo lake kwa miaka mitatu sasa kuna miradi haijatekelezwa licha ya kutengewa fedha.

"Sasa kama hamuwalipi hao wakandarasi hii miradi itakamilikaje, wananchi wanapata shida ya maji, nakuomba uje wewe mwenyewe uwaeleze kwanini miradi haijakamilika," alisema.

Lubeleje alisema yeye hawezi kukubali kukosa kura kwenye vijiji ambavyo havina maji kwenye jimbo lake kwasababu miradi haijakamilika.

"Wizara iliahidi kuchimba visima jimboni kwangu mpaka sasa hakuna kilichofanyika, hizo hela zilizotengwa zilienda wapi," alihoji.

Aliomba miradi inayopangwa na fedha zinazopitishwa na Bunge ziende kama inavyopangwa.

"Maji ni siasa kama ukiahidi kijiji kitachimbiwa kisima na hakuna kilichofanyika, tutapata tabu na uchaguzi ni mwaka kesho jamani," alisema.

Kadhalika, Mbunge wa Igalula (CCM), Mussa Ntimizi, alionyesha masikitiko yake kwamba kuna mradi wa kutoka maji Ziwa Victoria jimbo hilo halimo.

"Nimeona kuna mradi wa miji 29 bado jimbo la Igalula halijaangaliwa, kuna miji inapelekewa maji kupitia mradi wa Ziwa Victoria lakini pia imewekwa kwenye mradi wa miji 29,"alisema.

Alisema jimbo hilo maji hayaendi na fedha zinazotengwa ni kidogo haziwezi kutekeleza miradi ya maji huku akisema kuna tangi la maji linapeleka maji Sikonge ambalo lipo umbali wa kilomita 15, lakini jimbo hilo halina maji.





Mwezeshaji wa Mafunzo ya kuimarisha udhibiti wa magonjwa ambukizi kati ya binadamu na wanyama kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine, Profesa, Rudovick Kazwala, akifundisha kwa vitendo namna ya kutumia vifaa vya kitaalam vya kinga binafsi, wakati wa mafunzo hayo kwa wataalamu wa sekta za afya kutoka mikoa wa Songwe na Mbeya, halmashauri zilizopo mipakani. Mafunzo hayo yamefadhiliwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa na kuratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu chini ya Dawati la Kuratibu Afya moja, mkoani Songwe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shein ataka bei za bidhaa kutopanda Ramadhani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Alhaj Dk.Ali Mohamed Shein, amewataka wafanyabiashara kuwa waadilifu na kupunguza bei za bidhaa na huduma nyinginezo katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Dk. Shein aliyasema hayo katika risala maalum aliyoitoa kwa wananchi kupitia vyombo vya habari katika kuukaribisha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ambao unatarajiwa kuanza leo au kesho kutokana na kuandama kwa mwezi.

Aliwataka wafanyabiashara kukumbuka kwamba kwa kufanya hivyo hawatapata hasara bali watazidi kupata fadhila za Mungu zinazoambatana na Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Aliwataka wafanyabiashara kuzingatia ubora wa bidhaa wanazowauzia wananchi na kuwa wanapaswa wahakikishe kwamba wanawauzia bidhaa ambazo hazijaisha muda wake wa matumizi.

Alieleza kuwa wanunuzi nao wanatakiwa wawe makini wanaponunua bidhaa kwa kuwa si jambo la busara kununua bidhaa iliyokwisha muda wake wa matumizi kwa kufuata urahisi wa bei kwa sababu urahisi huo ni gharama kubwa kwa afya zao.

Aidha, aliwataka wakulima waendelee na ustaarabu pamoja na utamaduni wao ule ule wa ustahamilivu na uadilifu kwa kujiepusha na tabia ya uvunaji na uuzaji wa mazao machanga.

Dk. Shein aliwataka wauzaji wa bidhaa kama matunda, samaki, mboga na nyinginezo waache tabia ya kuuza bidhaa zao maeneo ya barabarani au kuziweka chini bila hata ya kutandika kitu kilicho safi.

Alisema kwamba wafanyabiashara ni lazima wafahamu kwamba kufanya biashara bila ya kuzingatia taratibu zilizowekwa kunaweza kuhatarisha usalama wa wapitao njiani, kuathiri ubora wa bidhaa hizo pamoja na afya za watumiaji wa bidhaa hizo.

Aidha, alizitaka taasisi zinazohusika zisimamie vyema shughuli za biashara masokoni na madukani, ili vitendo vya ghilba kwa wananchi ambao ndio wanunuzi na watumiaji wakubwa wa bidhaa visiendelee.

Alisema kuwa mwezi wa Ramadhani ni mwezi wa kuoneana huruma na kufanyiana hisani, hivyo wananchi wazidishe imani na huruma ili waweze kuitekeleza ibada ya saumu bila ya bughudha na usumbufu.

# Taarifa ya utekelezaji ilani ya CCM yazua taharuki

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

UONGOZI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kaskazini Unguja, umetakiwa kuwaunganisha Mbunge wa Jimbo la Donge na Mwakilishi wa Jimbo hilo ili kulinusuru jimbo hilo katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 kuendelea kuwa mikononi mwa CCM.

Hayo yalielezwa na wananchi wa Jimbo la Donge wakati wakizungumza na waandishi wa habari baada ya kumalizika kwa mkutano mkuu wa CCM wa jimbo hilo, ambao ulizua taharuki kutokana na wajumbe kuikataa taarifa ya utekelezaji wa ilani ya CCM iliyowasilishwa na Mbunge wa Jimbo hilo, Sadifa Juma Khamis.

Usi Ramadhan Kombo, alisema wananchi wa Donge wana masikitiko makubwa kuona viongozi wao wakuu wa jimbo hawaelewani wakati wanatoka chama kimoja.

Alisema kutoelewana kwa viongozi hao kumewafanya wananchi kuwa na makundi kati ya wanaomuunga mkono mbunge wanaomuunga mkono mwakilishi.

Alisema hatua hiyo imewafanya viongozi hao kutofanya kazi pamoja katika kulileta maendeleo jimbo hilo tangu walipowachagua. "Tunauomba uongozi wa CCM Mkoa wa Kaskazini kufanya jitihada za kuwaunganisha viongozi wetu, maana hatujui sababu ya wao kutoelewana wakati wote ni wana-CCM," alisema.

Riziki Simai, alisema viongozi hao wamewatumia wafuasi wao kulivuruga jimbo kutokana na kambi na makundi waliyonayo.

Alisema kama viongozi hao hawatokua na maelewano, kuna uwezakano wa kulipoteza jimbo hilo katika uchaguzi mwaka 2020. Mjumbe wa Halmashauri Kuu Taifa (NEC), Abeid Muhamed Khamis, aliwataka wananchi na viongozi wao wakiwamo mbunge na mwakilishi kuacha tofauti zao na kuachana na makundi.

"Tukiwa kila mmoja na lake hatutofika pahala kwani umoja ni nguvu utengano ni dhaifu...jimbo lina historia kubwa, ni ng'ome ya CCM, hivyo ni vyema kuiendeleza historia hiyo, "alisema.

Alieleza kuwa ripoti ya Mbunge huyo imeonyesha mambo mengi ambayo hayamo katika kipindi cha utekelezaji wa ilani ya CCM kwa kipindi cha kuanzia 2015 hadi 2019, badala yake mbunge huyo alieleza mambo ambayo aliyafanyaka katika kipindi chake cha mwanzo cha 2010 hadi 2015.

Alisema kuwa mbunge anatakiwa kuiandaa tena ripoti hiyo na kuiwasilisha tena kwa wajumbe ili iweze kuwasilishwa na kujadiliwa tena na hatimae wajumbe wafanya maamuzi ya kuipitisha au kutoipitisha ripoti hiyo.

Mbunge Sadifa, alisema kukataliwa kwa ripoti hiyo ni moja ya changamoto katika siasa kwa kuwa yote aliyoyaeleza katika ripoti hiyo ndiyo aliyoyatekeleza katika uongozi wake.

Alieleza masikitiko yake kuwa walioshiriki mkutano huo baadhi yao sio wajumbe halali wa mkutano huo na waliandaliwa kwa makusudi kwa lengo la kufanya fujo.

Mbunge huyo alikiri kutokua na mahusiano na Mwakilishi, Dk Khalid Salum Muhammed, ambaye alisema hupo tayari kukutanishwa na mwakilishi huyo ili kufanya kazi pamoja.

# Huduma bora kwa wajawazito

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa Mjini Magharibi Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, amewataka wakunga na wauguzi kuendelea kutoa huduma bora kwa wajawazito ili kuhakikisha wanajifungua salama na kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi.

Akizungumza na wakunga na wauguzi katika Maadhimisho ya Siku ya Wakunga Duniani ambayo kwa Zanzibar yalifanyika uwanja wa Mapinduzi Square Michenzani, aliwataka wafanyakazi hao mbali na kusimamia usalama wa wajawazito na watoto wakati wa kujifungua, pia wana jukumu la kulinda maadili ya kazi zao ya kutotoa siri za wagonjwa wanaowahudumia.

Ayoub alisema serikali inaendelea na juhudi zake za kuweka mazingira bora katika wodi za kujifungua na kutoa elimu kwa wafanyakazi wa kada tofauti kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utendaji wa kazi.

Alisema Serikali imeimarisha huduma katika vituo vya afya vijijini ili viweze kutoa huduma za mama na mtoto hivyo amewashauri wajawazito kuvitumia vituo vya karibu ili kupunguza msongamano katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja.

Akitoa maelezo kuhusu siku ya wakunga duniani, Mwenyekiti wa Baraza la Wauguzi na Wakunga Zanzibar, Amina Abdulkadir, alisema lengo la maadhimisho hayo ni kuwaunganisha wafanyakazi wa kada hiyo katika kujipima ili kuona mafanikio na changamoto zinazowakabili.

Alisema hivi sasa mataifa yaliyomo katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati zimekubaliana kuwa mtaala mmoja wa masomo ya wauguzi na wakunga katika kuhakikisha huduma zinazotolewa zinakuwa sawa katika nchi hizo.

Naye Katibu wa Jumuiya ya Wauguzi Zanzibar, Omar Abdalla Ali, alisema upungufu wa wafanyakazi na vitendea kazi katika kada ya ukunga na uuguzi unazorotesha ufanisi wa kazi katika hospitali na vituo vingi vya afya Zanzibar na kusababisha malalamiko kutoka kwa wananchi wanaofika kupata huduma.

# Waajiri sasa waelekezwa usalama mahali pa kazi

**Na Gwamaka Alipipi**

WAAJIRI nchini wametakiwa kuzingatia utekelezaji wa Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi pamoja na sheria zingine za kazi ili kuboresha mazingira ya kazi kama walivyokumbushwa katika kilele cha siku ya Wafanyakazi Duniani na Rais John Magufuli.

Kaimu Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Afya na Usalama Mahali pa Kazi (OSHA), Khadija Mwenda, alitoa wito huo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari akikazia agizo la Rais Magufuli kwa waajiri kuhusu utekelezaji wa sheria ya OSHA ya mwaka 2003 alilolitoa wakati wa sherehe ya Siku ya Wafanyakazi Duniani mkoani Mbeya.

Sheria hiyo ya OSHA imelenga kuwalinda wafayakazi dhidi ya madhara mbalimbali yanayoweza kuwapata wakiwa kazini.

"Kuna kila sababu kwa waajiri hao kuzingatia agizo hilo la Rais kwa kuwa msingi wa utekelezaji wake upo kisheria na kwamba kinyume cha hapo na ukiukaji wa makusudi wa sheria hiyo iliyoanzishwa kwa lengo la kulinda afya na usalama wa wafanyakazi wawapo kazini," alisema Mwenda.

Alisema waajiri hawanabudi kutekeleza matakwa mengine ya kisheria ikiwamo kutoa mikataba ya ajira na kuruhusu uwapo wa vyama vya wafanyakazi katika sehemu za kazi.

Wakati wa kilele cha Siku ya Wafanyakazi Duniani mkoani Mbeya, Rais Magufuli aliwataka waajiri na wamiliki wa sehemu za kazi kuzingatia utekelezaji wa sheria za afya na usalama kazini, hatua itakayosaidia kuboresha mazingira ya kazi kwa kuyafanya kuwa mahali salama zaidi kwa wafanyakazi.

Kauli hiyo ya Rais ilikuwa inajibu hoja mbalimbali zilizotolewa katika hotuba ya Shirikisho Huru la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA) iliyowasilishwa katika sherehe hizo na Katibu Mkuu wa Shirikisho hilo, Dk. Yahya Msigwa, ambaye pamoja na mambo mengine alibainisha uwapo wa baadhi ya waajiri ambao hawazingatii masharti ya OSHA inavyoagiza.



Meneja wa Mradi wa Majengo ya viwanda darasa wa SIDO, Mhandisi Omary Kitiku (kulia), akitoa maelezo kwa Mkurugenzi Mkuu wa SIDO, Prof. Sylvester Mpanduji (wapili kulia), juu ya maendeleo ya mradi wa majengo darasa ya viwanda kabla ya makabidhiano rasmi ya majengo hayo mkoani Dodoma. Watatu kulia ni Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa SUMA JKT.

# Waziri atoa angalizo hosteli za watalii porini

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, ameuagiza uongozi wa Pori la Swagaswaga mkoani Dodoma, kumsimamia Mkandarasi anayejenga Hosteli ya kulala watalii wapatao 77 kutokana na Mkandarasi huyo kuwa na rekodi isiyoridhisha ya kutokumaliza majengo ya serikali.

Pia, Ameutaka Uongozi huo kuwa makini na vifaa vya ujenzi anavyovitumia Mkandarasi huyo katika ujenzi wa jengo hilo utakaogharimu zaidi ya kiasi cha Sh. milioni 250 baada ya kubainika kuwa baadhi ya tofali zinazotumika kuwa chini ya kiwango. Hayo yamesemwa na Naibu Waziri huyo wakati alipotembelea ujenzi wa hosteli yenye uwezo wa kuhudumia watalii 77 kwa mara moja inayojengwa katika Pori hilo katika wilaya ya Chemba mkoani Dodoma na kutaka hosteli hiyo ikamilike kwa muda uliopangwa na kwa kiwango chenye ubora kulingana na thamani ya fedha iliyotolewa.

Akiwa katika ziara hiyo, Kanyasu alifika katika jengo hilo na kujionea tofali zilizoandaliwa kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo zikiwa zimekatika vipande vipande. Hali hiyo imemfanya Kanyasu kuagiza tofali hizo zikapimwe kwenye mamlaka husika kama zinakidhi viwango kwenye ujenzi wa jengo hilo.

Kufuatia hali hiyo, Naibu Kanyasu ameuthadhalisha uongozi huo kuwa makini na hatua za ujenzi wa jengo hilo la sivyo wataingia kwenye matatizo makubwa.

"Nawaagiza simamieni kwa kila hatua za ujenzi wa majengo hilo, mambo yakiharibika hamtakuwa salama, ni lazima tuhakikishe thamani ya fedha inaendana na jengo halisi," alisisitiza Kanyasu.

Aidha, aliutaka uongozi huo uhakikishe vifaa vya ujenzi anavyovitumia Mkandarasi huyo ni vile ambavyo vimeandika kwenye mkataba na si vinginevyo.

Katika hatua nyingine, Kanyasu alitembelea jengo la ofisi za Pori hilo ambalo linaendelea kujenga katika eneo la Kwa mtoro na kuutaka uongozi huo kusimamia kwa ukaribu majengo yote yanayoendelea kujengwa kwa ajili ya manufaa ya Pori hilo.

# Wataka udhibiti uuzaji ramani

**Na Gwamaka Alipipi**

CHAMA cha Wabunifu Majengo Tanzania (AAT), kimeiomba serikali kuingilia kati biashara ya uuzwaji holela wa ramani za nyumba unaofanywa na watu wasio na taaluma, kwani ndiyo chanzo cha kuanguka kwa majengo nchini.

Rais wa chama hicho, Henry Mwoleka, alitoa rai hiyo jijini Dar es Salaam wakati wa semina endelevu ya 12 ya ATT ambapo alieleza kumekuwapo na wafanyabiashara makanjanja wanaouza ramani za nyumba zisizokuwa na viwango bora.

"Tunakabiliwa na changamoto nyingi, lakini kubwa ni uuzwaji wa ramani za nyumba kama njugu, Watanzania wengi sasa hivi wanakimbilia kununua ramani hizo kutokana na kuuzwa kwa bei nafuu," alisema Mwoleka.

Alisema ramani hizo zinauzwa kati ya Sh. 20,000 hadi 50,000 kwa kuwa siyo halisi, wakati bei ya ramani iliyochorwa kwa viwango vyenye ubora huuzwa kuanzia Sh. milioni moja na kuendelea.

Mwoleka alisema ATT inaomba sheria izingatiwe kwa wahusika wanaouza ramani hizo, kwa kuwa kwa kufanya hivyo kunadidimiza taaluma ya ubunifu majengo nchini.

Alisema changamoto nyingine wanayokabiliana nayo ni kutokuwapo kwa ushirikiano kati ya serikali na sekta binasfi katika ufanyaji kazi, hususani kwenye ubunifu majengo.

Alisema changamoto nyingine ni wabunifu majengo kutotambulika katika sera za serikali, pamoja na kutokuwa na mifumo thabiti ya utendaji kazi.

"Wabunifu majengo hatutambuliki, tunaomba tutambulike, wanaotengeneza sera watutambue, tunataka tuwe na jukwaa la kuongea na serikali moja kwa moja," alisema Mwoleka.

Kadhalika, alisema hadi kufikia Desemba 31, mwaka jana idadi ya wabunifu majengo waliokuwa wamesajiliwa nchini walikuwa 456, na kampuni za ubunifu majengo 473.

Aliongeza kuwa ATT kimekuwa na uhusiano mzuri na vyuo vikuu vya nchini na nje ikiwamo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Chuo cha ufundi Berlin Ujeruman.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni, Ng'wilabuzu Ludigija, alisema ni kweli kwa sasa kuna changamoto katika ujenzi wa majengo nchini kwa sababu serikali imekuwa ikijielekeza katika ujenzi wa viwanda.

Alisema hata hivyo, serikali inatambua mchango wa sekta ya ujenzi katika kujenga uchumi wa nchi.

HABARI KIMATAIFA

## Maduro aliandaa jeshi kupambana na Marekani

**CARCAS,** Venezuela

RAIS wa Venezuala, Nicolas Maduro amevitaka vikosi vya jeshi kujiweka tayari kwa mapambano dhidi ya Marekani, wakati wafuasi wa kiongozi wa upinzani Juan Guaido wakikusanyika kwenye kambi za jeshi kujaribu kutafuta uungwaji mkono.

Rais Maduro (pichani) ameliamuru jeshi kujiandaa wakati wowote na kuilinda nchi hiyo kwa silaha iwapo Marekani itajaribu kuchukua hatua za kijeshi.



Venezuela ni taifa lililopo Amerika ya Kusini lenye utajiri mkubwa wa mafuta. Katika kusisitiza kuwa jeshi linaendelea kuunga mkono utawala wake wa kijamaa, Rais Maduro alitoa hotuba kupitia televisheni akiwa pamoja na waziri wake wa ulinzi sambamba na vikosi vya wanajeshi 5,000.

Harakati za Guaido zilipata uungwaji mpya juzi kutoka kwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo, alietoa mkanda wa video akiwahimiza raia wa Venezuela kuchukua hatua, huku akisema wakati wa mabadiliko kwa taifa hilo umewadia. **DW**

## Korea Kaskazini yarusha makombora

**PYONGYANG,** Korea Kaskazini

KOREA Kaskazini imerusha makombora ya kwanza tangu mwaka 2017.

Msururu wa makombora ya masafa mafupi yalirushwa Jumamosi na kuangukia karibu na Bahari nchini Japan.

Iwapo itathibitishwa kuwa ni uzinduzi wa makombora ya masafa mafupi, yatakuwa ni ya kwanza kurushwa na Korea Kaskazini tangu uzinduzi wake wa Novemba 2017.

Baada ya uzinduzi huo, Korea Kaskazini ilitangaza kuwa uwezo wake wa kinyuklia umekamilika na ikakubali kuanzisha tena mazungumzo na Marekani pamoja na Korea Kusini.

Msemaji wa Ikulu ya Marekani, Sarah Sanders alisema: "Tunazo taarifa kuhusu hatua za Korea Kaskazini za usiku huu. Tutaendelea kuzifuatilia".

Korea Kusini imesema makombora hayo yalirushwa kutoka mji wa Wonsan wa Korea Kaskazini majira ya saa tatu asubuhi.

Korea Kusini imeeleza kwamba inafanya uchunguzi kuhusu makombora hayo, ikishirikiana na Marekani.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Korea Kusini, Kang Kyung-wha alisema Korea Kaskazini inalazimika kusitisha shughuli zake za kinyuklia iwapo inataka kuondolewa vikwazo ilivyoyowekewa.

Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Korea Kaskazini, Choe Son Hui ameonya juu ya matokeo yasiyofurahisha iwapo Marekani haitobadilisha msimamo wake kuhusu vikwazo vya kiuchumi ilivyoiwekea nchi yake. **DW**

# Al Bashir kuhojiwa kwa utakatishaji fedha, ugaidi

**KHARTOUM,** Sudan

MWENDESHA mashitaka mkuu wa Sudan ameanza kumhoji aliyekuwa Rais wa nchi hiyo, Omar al Bashir, kwa madai ya kutakatisha fedha na kufadhili ugaidi.

Uamuzi huo umefanyika wakati wananchi wa Sudan wakifanya maandamano mjini Khartoum wakidai serikali ya kiraia.

Taarifa kutoka katika ofisi ya mwendesha mashitaka mkuu zimethibitisha kwamba, Kaimu Mwendesha Mashitaka Mkuu, Jenerali Al Waleed Sayyed Ahmed ameamuru Al Bashir ahojiwe kwa mujibu wa sheria dhidi ya kutakatisha fedha na kugharamia ugaidi.

Marekani imeiondolea Sudan vikwazo vya kibiashara Oktoba, 2017 baada ya kudumu kwa miaka 20. Hata hivyo imeendelea kuiweka kwenye orodha ya mataifa yanayounga mkono ugaidi wa kimataifa pamoja na Iran, Syria na Korea ya Kaskazini.

**Pande hizo mbili zimekubaliana kuunda baraza la pamoja litakalokuwa na raia na wanajeshi lakini zinazozana juu ya muundo wa baraza hilo.**

Sudan iliingizwa katika orodha hiyo kwa sababu ya tuhuma kuwa ina mfungamano wa pamoja na wanamgambo wa itikadi kali, Muasisi wa mtandao wa kigaidi wa Al Qaida Osama Bin Laden ambaye aliishi Sudan kati ya mwaka 1992 na 1996.

Jenerali Abdel Fattah al Burhane ambaye kwa sasa anaongoza baraza la kijeshi la mpito nchini Sudan alisema ujumbe wa nchi hiyo utakwenda hivi karibuni Washington kuzungumzia namna ya kuitoa Sudan katika orodha ya nchi zinazounga mkono ugaidi.

Wakati huo huo, wiki tatu baada ya Omar al Bashir kupinduliwa na wanajeshi, umati wa waandamanaji walijazana katika eneo linalozunguka makao makuu ya jeshi mjini Khartoum kwa kile kilichotajwa kuwa ni maandamano makubwa ya kudai serikali ya kiraia.

Waandamanaji walikusanyika kwa wingi kuliko siku zingine wakiwa katika njia zote na daraja zinazoelekea katika jengo hilo lililoko kati kati ya Mji Mkuu wa Khartoum, wakati ambapo mazungumzo kati ya waandamanaji na watawala wa kijeshi yanaendelea kukwama.

Pande hizo mbili zimekubaliana kuunda baraza la pamoja litakalokuwa na raia na wanajeshi lakini zinazozana juu ya muundo wa baraza hilo.

Wakati ambao waandamanaji wanadai raia wadhibiti taasisi huyo, wanajeshi wao wanataka idadi ya wanajeshi wawe wengi katika baraza hilo la pamoja. Waandamanaji wamewakabidhi wanajeshi mapendekezo kuhusu muundo wa utawala wa kiraia nchini Sudan. **DW**



Wanaume wakibeba majeneza yaliogunduliwa ya wahanga 84,437 wa mauaji ya kimbari ya 1994, tayari kwa ajili ya kuzikwa mjini Kigali. **PICHA: AFP**

# Afrika kusaidiwa kupambana na ugaidi

**OUGADOUGU,** Bukina Faso

KANSELA wa Ujerumani, Angela Merkerl, ametangaza msaada wa kijeshi, kiuchumi, kupambana na ugaidi pamoja na kuboresha uwekezaji kwa nchi za Afrika Magharibi.

Merkerl ameyasema hayo akiwa Niger baada ya kumaliza ziara ya siku moja nchini Bukina Faso.

Akiwa mjini Ougadougu, kiongozi huyo wa Ujerumani alihudhuria mkutano wa viongozi wa mataifa matano ya kanda ya Sahel wa kundi la G5, na kujadili namna ya kuimarisha kikosi maalum cha kupambana na ugaidi katika kanda hiyo ya Afrika magharibi.

Merkel aliahidi msaada wa dola milioni 20 kwa Burkina Faso, pamoja na msaada wa Euro milioni 60 kwa kundi la mataifa matano ya Sahel G5 yaliyounda kikosi cha pamoja cha wanajeshi elfu tano kupambana na ugaidi katika ukanda wao.

Akiwa nchini huyo, Merkel alisema Ujerumani itaendelea kuimarisha misaada zaidi kwa kutoa vifaa na mchango wa Euro milioni 10, vile vile kutakuwa na msaada wa ushauri kupitia jeshi la Ujerumani utaogharimu kati ya Euro milioni saba hadi 10.

Merkel ana mipango pia ya kuipatia Niger Euro milioni 35 kwa lengo la kuhamasisha uwekezaji binafsi katika kanda hiyo ya Afrika Magharibi kwa msaada wa serikali ya Ujerumani.

"Kwa upande wa ushirikiano wa maendeleo tayari tumetoa msaada na ninadhani msaada huo umeanza kufanya kazi vyema," alisema Merkel.

"Lengo la Ujerumani ni kusaidia kubuni nafasi za ajira bora zaidi kwa ajili ya vijana wa Afrika ili kupunguza hali ya umaskini pamoja na kukabiliana na ukosefu wa utulivu wa kisiasa na ghasia, mambo ambayo yanawalazimisha waafrika wengi kukimbilia Ulaya"

Burkina Faso ni Mwenyekiti wa zamu wa kundi la G5, ambapo Merkel alihudhuria mkutano wa viongozi wa kundi hilo uliohudhuriwa na Marais Ibrahim Boubacar Keita wa Mali, Mohamed Ould Abdel Aziz wa Mauritania, Mahamadou Issoufou wa Niger na Idriss Deby wa Chad.

Katika mkutano huo Merkel alitangaza msaada wa Ujerumani wa dola za Marekani milioni 51 ili kuweza kusaidia kuimarisha usalama katika kanda hiyo. **VOA**

# Mama Maria: Fanyeni maombi muongezwe mishahara

**Na Beatrice Moses**

MKE wa Baba Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, Mama Maria Nyerere, amewataka Watanzania kuwaombea viongozi wa kitaifa ili wafanye kazi vizuri, kiwango cha uchumi kiongezeke na mishahara iongezwe.

Aliyasema hayo juzi wakati wa matembezi ya kuombea nchi amani, yaliyoendana na maadhimisho ya Jubilee ya miaka 50 kwa Kituo cha Huduma ya Maombezi.

"Tunaomba sala hii pia ikawe tumaini kwa wafanyakazi wote, muendelee kuwa wavumilivu kwa maombi mnayotoa serikalini kuhusu kuongezewa kipato ili mwakani kiweze kuongezeka," alisema Mama Maria.

Aliwataka wananchi waendelee kumuombea Rais John Magufuli pamoja na mawaziri wake na viongozi wengine, ili waweze kulitumikia taifa vyema.

Mama Maria alisema viongozi ndiyo wenye jumukumu la kusimamia maendeleo, wakati viongozi wa kiroho wapo ili kuhamasisha faida ya kumtangulia Mungu mbele katika kila jambo.

Alisema kwa sala hiyo pia wanaliombea taifa, kanisa na ulimwengu mzima ili uweze kuwa na amani na kuwa na shukrani kwa Mungu kwa kuendelea kuijalia nchi amani na pia kuweka Safina.

"Tunaposema Safina maana yake ni chombo cha kuokoa roho, kuna wengine wamekuja hapa wana magonjwa yasiyokuwa na dawa, lakini wafanyiwa maombi hapa," alisema Mama Maria.

Alisema nchi inahitaji kuwa na watu watulivu, kwa kuwa hata vijana wenye hofu ya Mungu wamejaa utulivu.

"Hata wanapotembea unawaona kabisa kuwa ni watulivu na wanyenyekevu, maombi yanaweza kubadilisha hata wale wanaoonekana wana tabia mbaya," alisema Mama Maria.

"Pia hata inapotokea uchaguzi mkuu tunaombea, ili Mungu atuchagulie viongozi wa Pendekezo lake," alisema.

Matembezi hayo yalihudhuriwa na waumini wengine wa kituo hicho kutoka nchi za Marekani na Uingereza.

Mwanzilishi wa huduma hiyo, Kasisi Felician Nkwera, alisema anashukuru Mungu imekuwa na inasaidia watu kupata uponyaji wa magonjwa na kutolewa pepo.

Alisema ni changamoto kubwa kupambana na shetani, lakini kwa nguvu zake Mwenyezi Mungu wanapata ushindi unaowapa nguvu ya kuendelea kutoa huduma hiyo bila kukata tamaa.

Matembezi hayo yaliyoanzia eneo la Tazara na kupita Barabara ya Mandela hadi kwenye kituo hicho cha maombezi kilichopo Riverside, Dar es Salaam.

wafuasi kadhaa wa huduma kutoka mikoa mbalimbali nchini, wakiwamo waumini wengine wa kituo hicho kutoka nchi za Uingereza na Marekani walijitokeza kuhudhuria matembezi hayo, huku wakiwa wamebeba sanamu ya Bikira Maria na mabago yaliyoandikwa ujumbe mbalimbali.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akimkabidhi cheti cha ushiriki Mkuu wa Mauzo wa Kanda ya Kati wa kampuni ya Vodacom Tanzania Plc, Grace Chambua, wakati wa maadhimisho ya miaka 10 ya UCSAF jijini Dodoma mapema wiki hii. Maadhimisho ya mfuko huo wa mawasiliano kwa wote yameadhimishwa na kauli mbiu ikiwa ni 'Mawasiliano kwa wote ni kichocheo cha kuufikia uchumi wa kati'. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Takukuru wamulika mradi wa maji Dar

**Na Beatrice Moses**

MRADI wa maji unaotarajiwa kunufaisha takribani watu 15,000 katika Kata ya Saranga jijini Dar es Salaam, umeelezwa kukumbwa na changamoto ya rushwa, iliyosababisha Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa(Takukuru) kuingilia kati.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Saranga, Godwin Muro, aliiambia Nipashe jana kuwa kuchelewa kukamilikika kwa wakati uliotarajiwa kwa mradi huo kumezua changamoto na malalamiko kutoka kwa wananchi.

"Hali hiyo ndiyo iliyosababisha maofisa wa Takukuru na Mkuu wa Wilaya kuja kukagua, siku tatu wamezunguka huku wakifuatilia, hata hivyo mimi nimejulishwa na Dawasa (Mamlaka ya Maji) kuwa upungufu wa vifaa ndiyo umesababisha kuchelewa kutolewa kwa huduma hiyo," alisema.

Muro alidai kuna baadhi ya vibarua waliopewa kazi za kuchimba mifereji ya kuchimbia mabomba wametajwa kuhusika kushawishi wananchi kuwapa rushwa ili wawachimbie na kuwapa mipira.

"Hao wanaokubali kununua vifaa hivyo au kuwalipa wachimbaji, wanapata gharama za bure kwa sababu utaratibu ni kwamba vyote vinaletwa na Dawasa kisha baada ya kuunganishiwa huduma, unaanza kulipia kupitia kwenye ankara yako," alisema.

Jonathan Mwakatobe, mkazi wa Saranga, alisema wameshangazwa kuona baadhi ya watu wamewekewa mabomba hadi kwenye makazi yao kwa upendeleo kutokana tu na kufahamiana baadhi ya maofisa wanaohusika na mradi.

"Tupo eneo moja lakini unashangaa mwenzako kawekewa bomba hadi nyumbani kwake, tena ni pana umbali mrefu wamevukwa majirani, tunafikiri anaweza kuwa ni mfanyakazi mwenzao wa Dawasa au anafahamiana nao, tunaomba serikali ikomeshe mambo haya," Mwakatobe alisema.

Meneja wa Dawasa Wilaya ya Ubungo, Passcal Fumbuka, alisema vifaa vimechelewa kufika lakini tayari vimewasili bandarini.

Alisema changamoto hiyo haijatokea Saranga pekee, bali kwenye kata 10 ambazo mradi huo unapita.

"Nimekuwa nikihubiri mara zote kwamba fedha ya serikali inapokelewa na kutolewa risiti, vijana wetu wanakuwa na sare na vitambulisho hivyo kuwabaini ni rahisi, gharama za mipira na vifaa vingine vinawekwa kwenye ankara, haipaswi kulipiwa kabla ya kufungiwa huduma hiyo," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kisare Makori, alizindua mradi huo Machi 22, mwaka huu na kueleza kuwa hatua hiyo ni utekelezaji wa ahadi ya serikali ya kuhakikisha inasogeza huduma muhimu karibu na wananchi.

# SUMA JKT yaikabidi Sido majengo viwanda

**NaMwandishi Wetu,** DODOMA

WAJASIRIAMALI nchini wametakiwa kuyatumia majengo ya viwanda darasa'Industrial sheds' yaliyojengwa katika mikoa mbalimbali lengo likiwa kuwekeza viwanda vidogo na vya kati vitakavyosimamiwa na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) ili kuendeleza na kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi wa kati na viwanda .

Akizungumza mara baada ya makabidhiano ya mradi wa majengo matatu ya viwanda kutoka kwa mkandarasi SUMA JKT yaliyofanyika katika eneo la mradi Kizota mkoani Dodoma, Mkurugenzi Mkuu wa SIDO, Prof.Sylvester Mpanduji, alisema kukamilika kwa mradi huu ni fursa sasa kwa wajasiriamali kupata maeneo ya kuweka viwanda ili kukuza sekta.

"Hii ni fursa kwa wajasiriamali wa mkoawa Dodoma kuyatumia majengo haya kuwekeza viwanda vidogo vitakavyokuwa chini ya uangalizi ili kufanya uzalishaji wenye tija na kukubaliwa sokoni na kupelekea kuzalisha wawekezaji wengi wa ndani," alisema Prof. Mpanduji.


Alisema majengo haya yamejengwa kwa fedha nyingi za Serikali, hivyo ni lazima kuhakikisha yanapata wapangaji watakao wekeza viwanda vyao lengo likiwa kukuza uzalishaji wa bidhaa zinanzotokana na mazao ya kilimo na mifugo.

"Kama SIDO tunajukumu la kutangaza majengo haya ambayoyamejengwa kwenye mikoa mitano ili kuhakikisha yanapata wajasiriamali na kufanikisha azma ya serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais John Magufuli ya kujenga uchumi kati na viwanda ifikapo mwaka 2025," alisema Prof. Mpanduji.

Mikoa ambayo tayari majengo ya viwanda darasa yamejengwa ni Mtwara, Manyara, Geita, Kagera na Dodoma. Alitoa wito kwa wajasiriamali katika mikoa hiyo kutembelea ofisi za SIDO ili wapatiwe utaratibu wa kuwekeza viwanda katika majengo hayo.

"Lengo letu ni kumwinua mjasiriamali kutoka katika daraja la chini la uzalishaji bidhaa na kufikia daraja la kati na hatimaye kuwa mwekezaji mkubwa kwa kuhakikisha bidhaa zake zinakidhi viwango vya ubora kupitia mamlaka husika za serikali," alisema Prof. Mpanduji aliishukuru serikali kutoa shilingi bilioni tano kwa mwaka wa fedha 2017/18 ambayo imewezesha ujenzi wa majengo ya viwanda darasa yapatayo kumi na moja katika mikoa mbalimbali nchini.

Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa SUMA JKT, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, ambaye aliyemwakilisha Mkuu wa JKT, Meja Jenerali Martin Busungu, aliishukuru SIDO na Serikali kwa kulipaJeshi kandarasi ya ujenzi wa majengo hayo na kuahidi kuendelea kufanya kazi nzuri iliyotukuka kwa maslahi na ustawi wa taifa.



# ZIDANE AFUNGUKA KUHUSU POGBA

# LACAZETTE AWANIWA BARCELONA




**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Alexandre Lacazette anawaniwa na Barcelona wakati wa kipindi cha majira ya joto, huku mshambuliaji wa Atletico Madrid, Antoine Griezmann bado akibaki kwenye rada za miamba hao wa Katalunya.

Sio siri kwamba, Barça inatafuta mshambuliaji mpya, huku klabu hiyo ikitafuta mrithi wa Luis Suarez, ambaye ana umri wa miaka 32, ambaye hatakuwa na misimu mingine mingi hapo Camp Nou.

Griezmann alikaribia kusajiliwa Barcelona kipindi cha majira ya joto kilichopita, kabla ya kughairi dakika za mwisho.

Lakini bado Barcelona wanamwania raia huyo wa Ufaransa kwa ajili ya kuimarisha kikosi chao.

Gazeti la Mundo Deportivo limeripoti kwamba Lacazette sasa ameingia kwenye rada za Barcelona ambaye thamani yake inatajwa kuwa ni euro milioni 65 hadi euro milioni 70.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 amekuwa kwenye kiwango cha juu zaidi hapo kwa washikabunduki, huku akifunga mabao mawili kwenye ushindi wa 3-1 dhidi ya Valencia kwenye mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya Kombe la Ligi ya Europa.

Na sasa amefikisha mabao 18 kwenye michuano yote aliyoifungia Arsenal msimu huu na kuendelea kuwa katika kiwango cha kuvutia zaidi.

## Ribery atangaza kuondoka

**MUNICH,** Ujerumani

KLABU ya Bayern Munich imetangaza kwamba, Franck Ribery hataongeza mkataba wake, hivyo atahitimisha miaka 12 ya Mfaransa huyo kukaa na miamba hao wa Bavaria.

Habari hizo zilikuwa zinatarajiwa kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36 akiungana na Arjen Robben kuondoka hapo kwenye miamba hao wa Bundesliga.

Tovuti rasmi ya klabu hiyo ya Bayern imethibitisha kwamba wachezaji wote wawili watapewa tuzo kwa mchango wao waliotoa kwa klabu hiyo katika mechi ya kuwaaga mwakani, huku mkataba wa Ribery utamalizika Juni 30.

"Wakati nilipokuja Bayern, ilikuwa ni ndoto iliyokuwa kweli. Haitakuwa kazi rahisi kusema kwa heri, lakini kamwe hatuwezi kusahau kwa kile tulichokipata kwa pamoja," amesema Ribery.

"Tumeshinda vitu vingi kwa pamoja kwa zaidi ya saa 20."

Akiwa amejiunga na klabu hiyo katika kipindi cha majira ya joto mwaka 2007 akitokea Marseille, Ribery amekuwa na muda wa mafanikio akishinda mataji nane ya Ligi na moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya, aliloshinda mwaka 2013, ambapo Ribery alitoa pasi ya mwisho kwa Robben kufunga bao la ushindi kwenye Uwanja wa Wembley.

Ribery amecheza jumla ya mechi 422 akifunga mabao 123 kwa miamba hao wa soka la Ujerumani.

"Franck na Arjen ni wachezaji wakubwa. FC Bayern inawashukuru wote kwa pamoja," alisema Mwenyekiti wa Klabu hiyo, Karl-Heinz Rummenigge.



## Spurs waingia vitani kumwania Van de Beek



**LONDON,** England

KLABU ya Tottenham, imeungana Bayern Munich na Borussia Dortmund kwenye mbio za kuwania kumsajili nyota wa Ajax, Donny van de Beek.

Beek anatajwa kuwa thamani yake ni pauni milioni 45 na Spurs inamtafuta mrithi wa Christian Eriksen ambaye anawaniwa na Real Madrid.

Donny van de Beek anaweza kujikuta akiwa pale kwenye dimba la Tottenham Hotspur msimu ujao.

Beek amekuwa akifuatiliwa kwa karibu na Tottenham ili kuziba pengo la Eriksen, ambaye atakamilisha uhamisho wake kwenda Real Madrid.

Hata hivyo, Spurs itakumbana na kikwazo kutoka kwa Bayern Munich na Borussia Dortmund, ambazo nazo zipo kwenye mbio za kuwania saini ya kiungo huyo.

Tottenham imekuwa na uhusiano mzuri zaidi na klabu hiyo ya Uholanzi kwa miaka ya hivi karibuni, ikiwa imewasajili wachezaji wake kama Eriksen, Jan Vertongen na Davison Sanchez.

Na sasa Spurs ipo katika wakati mzuri wa kusajili De Beek ambaye atakuwa na kazi rahisi tu ya kutua hapo England. Kocha wa Spurs, Mauricio Pochettino ameahidi kutaka kuimarisha kikosi chake kwa kuwasajili wachezaji kadhaa nyota.

# Barcelona yachezea kichapo La Liga




**BARCELONA,** Hispania

MABINGWA wapya wa Ligi Kuu Hispania, La Liga, Barcelona walikumbana na kipigo cha kushtukiza kutoka kwa Celta Vigo baada ya kuwapumzisha Lionel Messi, Luis Suarez na Gerard Pique.

Maxi Gomez alianza kwa kufunga bao la kwanza kwa Celta baada ya bao lao la awali kukataliwa na teknolojia ya uamuzi ya video, VAR.

VAR baadae iliwapa penalti Celta na ikafungwa na Iago Aspas na kupata bao lao la pili.

Barca itacheza na Liverpool kesho Jumanne katika mchezo wa marudiano wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, baada ya mchezo wa kwanza kuibuka na ushindi wa mabao 3-0.

Kikosi hicho cha Ernesto Valverde ambacho pia kilikuwa bila ya nyota, Ivan Rakitic, Sergio Busquets na Jordi Alba, kilimpoteza Ousmane Dembele aliyeumia dakika za mwanzo.

Iliwachukua hadi dakika ya 28 kuweza angalau kupiga shuti la kwanza langoni mwa wapizani wao, huku golikipa wa Barca, Jasper Cillessen akiokoa hatari kadhaa langoni mwake.

Celta wangeweza kufunga ndani ya dakika tano za mwanzo za kipindi cha pili wakati Nestor Araujo alipopiga mpira kwa kichwa na ukaokolewa na Cillessen.

# KLOPP: LIVER ILIPIGANA KIUME KWA NEWCASTLE



**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amekisifia kikosi chake baada ya ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Newcastle, huku timu yake ikiendelea kuwa kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England pamoja na Manchester City.

"Tulipigana kwa moyo mmoja na hatimaye tukapata ushindi, kwa uhakika kucheza kwetu kwa moyo ndio kulikochangia ushindi huu," alisema Klopp.

Bao la kichwa la Divock Origi aliyetokea benchi dakika ya 86 ndilo lililowahakikishia Liverpool ushindi na kuendeleza presha kwa City katika mbio za ubingwa wa ligi hiyo.

Kikosi hicho cha Klopp kwa sasa kina pointi 94 kileleni mwa msimamo ikiwa imewatangulia pointi mbili City, ambayo leo Jumatatu inacheza na Leicester City.

Katika mchezo wa mwisho wa ligi hiyo itakayopigwa Mei 12 mwaka huu, Liverpool itacheza na Wolverhampton Wanderers huku City ikicheza na Brighton.

"Tulipigana na naamini katika mechi ya mwisho pia tutapigana kuhakikisha tunaondoka na pointi zote tatu ili kuhakikisha tunautwaa ubingwa.

# *Salah hatihati kuivaa Barcelona*




**LIVERPOOL,** England

KIKOSI cha Liverpool ambacho kiko chini ya Jurgen Klopp kinaweza kuwa bila ya nyota wake, Mohamed Salah katika mchezo wa pili wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Barcelona.

Salah raia wa Misri aliumia kwenye mchezo wa juzi Jumamosi wa Ligi Kuu England wakati Liverpool wakiibuka na ushindi wa 3-2 dhidi ya Newcastle.

Klopp alisema kwamba ni haraka mno kusema kama Salah hatakuwa fiti kucheza dhidi ya Barca.


"Tumesikia, aliumia kwenye paja," alisema Klopp. "Alianguka uwajani, lakini kwa sasa ni mapema mno kusema kama ataukosa mchezo dhidi ya Barcelona.

"Bado tuna muda wa kumwangalia na madaktari watasema kama ataweza kucheza dhidi ya Barcelona au la."

Liverpool itakuwa bila ya mshambuliaji raia wa Brazil, Roberto Firmino katika mchezo huo dhidi ya Barcelona.

Firmino, ambaye aliumia misuli ya paja, hakuwamo kwenye mchezo wa Jumamosi dhidi Newcastle.

# DONDOO SOKA MAGAZETI ULAYA



# ZIDANE AFUNGUKA KUHUSU POGBA

**●●● Mfaransa huyo amesema kila kitu kitakuwa wazi baada ya msimu huu...**

**MADRID,** Hispania

KOCHA, Zinedine Zidane, amefunguka kuhusu tetesi za uwezekano wa kiungo wa Manchester United, Paul Pogba kujiunga na Real Madrid kupitia neema ya usajili wa vitita vizito unaotajwa kufanywa na kocha huyo.

**Zidane amesema kuwa anasikia yote yanayozungumzwa kuhusu Pogba na safari ya kuelekea Madrid, lakini amezitaja taarifa hizo kuwa ni upuuzi ambao hataki kujihusisha nao.**

"Pogba ni mchezaji mzuri, mchezaji ninayemfahamu, lakini ni hivyo tu. Sitaingia kwenye mambo hayo, hayo ni upuuzi," amesema Zidane.

"Kama utaniuliza mimi kuhusu Pogba, nitakwambia ni mchezaji wa Manchester United. Ni mchezaji mzuri lakini ni wa Manchester United," aliongeza.

Zidane alisema kuwa watafahamu zaidi kitakachotokea baada ya msimu kuisha.

Katika hatua nyingine, Zidane amewashusha presha mashabiki wa Real Madrid wenye kiu ya kuona usajili utakavyofanyika akiwaeleza kuwa huenda suala la usajili mkubwa likafanyika au lisifanyike wakati huu.

Wakati huo huo, Kaka wa mchezaji wa Manchester United, Florentin Pogba amesema kuwa ni suala la kusubiri wakati kwa mdogo wake kujua kama ataondoka ndani ya Manchester United kwenda Real Madrid ambapo amekuwa akihusishwa kwenda.

Mpaka sasa kocha wa Man United, Ole Gunnar Solskjaer ameshindwa kuelewa kama Pogba mwenye miaka 26 atabaki kwenye kikosi chake msimu ujao.

"Kwenye mpira jambo lolote linaweza kutokea, ila kwa sasa sijui nini kinaendelea kwa Pogba na Manchester United.

"Leo ninaweza kukwambia jambo hili na kesho kikatokea kitu kingine, haya yote yatakuwa wazi baada ya muda kupita, tusubiri na tuone kama ataondoka ama atabaki," amesema.

## ZISIKUPITE

### MOURINHO AITEGA ROMA

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Jose Mourinho amepewa ofa ya mkataba wa miaka mitatu na klabu ya Roma, lakini Mreno huyo amewaeleza kuwa atakuwa tayari kujiunga na klabu hiyo endapo itafanikiwa kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao. ***(Mail)***

### LACAZETTE ANUKIA BARCA

BARCELONA inajipanga kuanza mchakato wa kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ufaransa na Arsenal, Alexandre Lacazette ambaye ana umri wa miaka 27 kwa dau la pauni milioni 70. ***(Sunday Express)***

### UNITED YAMBANA DE GEA

GOLIKIPA wa Timu ya Taifa ya Hispania, David de Gea (28), amepewa muda wa wiki moja kufanya uamuzi kuhusu hatima yake ndani ya kikosi cha Manchester United. ***(Sun on Sunday)***

### NAVAS KUTUA UNITED

MANCHESTER United inatarajia kuangalia uwezekano wa kumsajili golikipa wa Real Madrid na raia wa Costa Rica, Keylor Navas (32), kutokana na kutofahamu hatima ya kipa wao wa sasa Mhispania De Gea. ***(Sunday Telegraph)***

### LIGT ATAKIWA BARCELONA

MANCHESTER City inajiandaa kupambana na Barcelona katika vita ya kuwania saini ya beki wa Ajax na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Matthijs de Ligt (19), ambaye thamani yake imetajwa kuwa ni pauni milioni 65. ***(Star Sunday)***

### WENGER ATAJWA NEWCASTLE

WAKALA ambaye anahusishwa na Arsene Wenger ameielekeza Newcastle United kama wanahitaji huduma ya kocha huyo wa zamani wa Arsenal endapo kocha wake wa sasa, Rafael Benitez atafikia uamuzi wa kuondoka. ***(Chronicle Live)***

### MATA KUBAKIA UNITED

KIUNGO wa Manchester United, Juan Mata ambaye alitarajiwa kurejea Hispania huku Athletic Bilbao wakionyesha kuumizwa baada ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 31 kupata mkataba wa mwaka mmoja wa kuendelea kuichezea timu hiyo ya Old Trafford. ***(Sunday Mirror)***

### POCHETTINO KUISUKA SPURS

KOCHA wa Tottenham, Mauricio Pochettino, ameelezwa kuwa atawezeshwa ili kuhakikisha anafanya usajili wa majina makubwa katika kipindi cha dirisha la majira ya joto. ***(Sun on Sunday)***

### VAN DE BEEK AGOMBEWA

TOTTENHAM Spurs imeungana na Borussia Dortmund pamoja na Bayern Munich katika mbio za kuwania saini ya kiungo wa Ajax na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Donny van de Beek (22). ***(Mail on Sunday)***

### GREALISH MATAWI JUU

THAMANI ya kiungo wa Aston Villa na Timu ya Taifa ya Vijana ya umri chini ya miaka 21 ya England (U-21), Jack Grealish imetajwa kuwa ni pauni milioni 60. ***(Sunday Mirror)***

## HABARI MICHEZO

# Polisi Tanzania waifuata Namungo

**Na Mwandishi Wetu**

HATIMAYE Polisi Tanzania nayo rasmi imepanda daraja na kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao baada ya juzi kuwafunga Boma FC mabao 2-1 katika mechi ya Ligi Daraja la Kwanza iliyochezwa kwenye Uwanja wa Chuo cha Ushiriki Moshi mkoani Kilimanjaro.

Ushindi huo wa juzi umewafanya "Maafande" hao wa Polisi Tanzania kufikisha pointi 47 na kuongoza katika Kundi A ikifuatiwa na Pamba FC ya jijini Mwanza ambayo ina pointi 42.

Polisi Tanzania imeungana na Namungo FC ya Lindi kutoka Kundi B ambayo imemaliza mechi zake ikiwa na pointi 49 kupanda daraja.

Katika mchezo wa mwisho wa hatua hiyo ya makundi, Pamba kutoka jijini Mwanza ikiwa ugenini kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid Arusha ilitoka dare ya goli 1-1 dhidi ya Arusha FC.

Mechi nyingine zilizochezwa juzi za ligi hiyo ilikuwa ni Geita Gold iliyopata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Arusha United wakati Dodoma FC iliwafungwa Mashujaa FC magoli 2-1 katika mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Transit Camp nayo ilipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Mgambo Shooting wakati Rhino Rangers ya Tabora ikiwa nyumbani ilitoka sare ya goli 1-1 dhidi ya Green Warriors ya Dar es Salaam.

Hatua inayofuata ni ya mechi za mtoano ambazo zitatoa timu zitakaposhuka daraja na kufahamu timu zitakazopanda daraja kutoka katika Ligi ya Mabingwa wa mikoa maarufu SDL.

**MSIMAMO LIGI KUU BARA**

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Yanga | 34 | 25 | 5 | 4 | 54 | 24 | 80 |
| 2. Simba | 30 | 24 | 3 | 2 | 61 | 12 | 78 |
| 3. Azam | 33 | 19 | 9 | 5 | 49 | 20 | 66 |
| 4. Mtibwa Sugar | 33 | 14 | 6 | 13 | 34 | 26 | 48 |
| 5. Lipuli | 34 | 12 | 12 | 10 | 30 | 31 | 48 |
| 6. Singida Utd | 34 | 11 | 10 | 13 | 26 | 33 | 43 |
| 7.Ndanda | 32 | 11 | 10 | 11 | 22 | 30 | 43 |
| 8. KMC | 33 | 9 | 15 | 9 | 33 | 25 | 42 |
| 9. TZ Prisons | 34 | 10 | 12 | 12 | 26 | 26 | 42 |
| 10. Coastal Union | 33 | 9 | 14 | 10 | 29 | 33 | 41 |
| 11. Mbeya City | 32 | 11 | 7 | 14 | 31 | 34 | 40 |
| 12. Kagera Sugar | 33 | 9 | 12 | 12 | 28 | 35 | 39 |
| 13. JKT Tanzania | 33 | 9 | 12 | 12 | 20 | 28 | 39 |
| 14. Ruvu Shooting | 34 | 9 | 12 | 13 | 31 | 40 | 39 |
| 15.Stand United | 33 | 11 | 6 | 16 | 30 | 41 | 39 |
| 16. Alliance | 34 | 9 | 11 | 14 | 26 | 38 | 38 |
| 17. Mwadui | 33 | 10 | 7 | 16 | 37 | 43 | 37 |
| 18. Biashara United | 33 | 9 | 10 | 14 | 25 | 31 | 37 |
| 19. Mbao | 33 | 9 | 10 | 14 | 19 | 33 | 37 |
| 20. African Lyon | 33 | 4 | 10 | 19 | 19 | 43 | 22 |

# SPORTPESA YAPONGEZWA KUILETA SEVILLA TANZANIA

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Utalii Tanzania, (TTB) imesema ujio wa timu ya Sevilla FC inayoshiriki katika Ligi Kuu Hispania ( La Liga) kupitia Kampuni ya SportPesa Tanzania utaendelea kutangaza vivutio mbalimbali vya hapa nchini.

**Sevilla inatarajia kuwasili nchini Mei 21 mwaka huu na kucheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Simba siku mbili baadaye kwenye Uwanja wa Taifa kufuatia mwaliko wa kampuni ya michezo ya kubahatisha nchini, SportPesa Tanzania.**

Meneja Masoko wa TTB, Geofrey Meena alisema kuwa kwa sasa wapo katika maandalizi ya maeneo ambayo wachezaji na viongozi wa timu hiyo watatembelea mara baada ya kuwasili hapa nchini.



Meena (pichani) alisema kuwa Sevilla ni maarufu sana duniani na wanaamini ujio wao utatangazwa na vyombo vya habari vya kimataifa na vya hapa nchini na kuendelea "kuipromoti" Tanzania nje ya mipaka yake.

"Huu ni mwendelezo wa juhudi ambazo kampuni ya michezo ya kubahatisha ya SportPesa Tanzania ya kuhamasisha michezo na kutangaza vivutio vya utalii. Ni fursa ambayo tulikuwa tunaisubiria. Tulifanikiwa wakati wa ujio wa timu ya Everton," alisema.

Alifafanua timu ya Everton mbali ya kutangaza nchi, kuhamasisha michezo, kukaa salama na kurejea Uingereza, imewafanya Sevilla kuja Tanzania kwa sababu wanajua watakuwa salama kama ilivyokuwa kwa wenzao.

"Kwa sasa ni vigumu kusema wachezaji na viongozi wa timu ya Sevilla watatembelea wapi. Maandalizi yanaendelea, ila wataweza kutembelea maeneo mbalimbali ya kitalii na kuona utamaduni wa nchi," alisema kiongozi huyo.

Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), iliiteua Simba kucheza na vigogo hao wa Hispania baada ya kufanya vema katika mashindano ya yaliyopita ya kuwania Kombe la SportPesa kwa timu za Tanzania.



Wanachama wa Yanga wakisikiliza maelekezo yaliyokuwa yanatolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi (Ally Mchungahela- hayuko pichani), kwenye Ukumbi wa Bwalo la Maafisa wa Polisi Oysterbay jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# *Waamuzi Bara wazidi kuzongwa*

**Na Isaac Kijoti,** MBEYA

LICHA ya kukubali uwezo mkubwa wa kikosi cha Simba pamoja na kipigo walichopata katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini hapa juzi, Kocha Mkuu wa Mbeya City, Ramadhani Nsanzurwimo amesema waamuzi ni tatizo Ligi Kuu Bara.

Mbeya City ikiwa uwanja wake wa nyumbani licha ya kuielemea Simba kipindi cha kwanza na kuongoza kwa bao 1-0, Wekundu wa Msimbazi hao walitokea nyuma kipindi cha pili na kushinda 2-1.

Akizungumza na Nipashe, Nsanzurwimo alisema anakubali kuwa mabao yalifungwa hayakuwa na matatizo isipokuwa faulo iliyotolewa ambayo ilizaa bao la pili kupitia kwa Kagere.

"Sikatai matokeo wala mabao, ila refa hakuwa makini na tatizo lilianzia kwa msaidizi wake namba moja (Michael Mkongwa kutoka Njombe), alishindwa kabisa kwenda na mchezo.

"Yeye aliona kabisa haikuwa faulo lakini akanyoosha kibendera namna hii soka la Tanzania itakuwa kazi kukua, sheria 17 hazikufuatwa kabisa," alisema kocha huyo raia wa Burundi.

Alisema anakubali uwezo mkubwa ulionyeshwa na kikosi cha Simba huku akiwapongeza wachezaji wake kwa kumiliki mchezo zaidi kipindi cha kwanza na kufanikiwa kupata bao la kuongoza.

"Simba ina uwezo mkubwa na wachezaji wazuri, lakini niwapongeze wachezaji wangu kwa kumiliki mchezo kipindi cha kwanza katika mechi hii ambayo waamuzi walifanya makosa mengi kinyume cha sheria 17 za soka," alisema.

Katika mechi hiyo, Mbeya City ambayo ilimiliki mpira zaidi kipindi cha kwanza, kama ingeendelea kushambulia mwanzo mwisho, ingeweza kupata mabao zaidi ya mawili, lakini ilipopata bao la kuongoza, ilicheza mchezo wa kujilinda zaidi na kutoa nafasi kwa Simba kuwashambulia.

# Michezo



Jumatatu Mei 6, 2019
Nipashe

Zidane afunguka kuhusu Pogba HABARI UK.30





Mshambuliaji wa Chelsea, Eden Hazard (kushoto), akikabwa na beki wa Watford, Adrian Mariappa, katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa jana jioni kwenye Uwanja wa Stamford Bridge. Chelsea ilishinda mabao 3-0. **PICHA: MTANDAO**

# Simba yanoga Bara

## Bao la Mganda Okwi lawafanya wabakize pointi mbili kuwafikia watani zao...

**Na Adam Fungamwango**

BAO pekee lililofungwa na mshambuliaji Mganda, Emmanuel Okwi, liliweza kuwapa ushindi Simba dhidi ya 'Maafande' wa Prisons katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya.

**Kwa matokeo hayo, yaliifanya Simba ifikishe pointi 78, mbili nyuma ya vinara Yanga, lakini mabingwa hao watetezi wakiwa na mechi nne pungufu za ligi hiyo inayotarajiwa kumalizika mwishoni mwa mwezi huu.**

Simba sasa imefanikiwa kuvuna pointi sita katika jiji hilo baada ya Ijumaa iliyopita kuichapa Mbeya City mabao 2-1 kwenye uwanja huo huo, hivyo kuondoka na ushindi kwenye mechi zote mbili.

Lilikuwa ni bao la dakika ya 11 la Okwi ambaye ni mshambuliaji mkongwe wa Simba na Timu ya Taifa ya Uganda (The Cranes).

Bao hilo alilifunga kutokana na mpira mrefu uliopigwa kutoka katikati ya uwanja na kumkuta mfungaji, aliyempiga chenga kipa, Aron Kalambo na kupiga shuti ambalo lilitambaa taratibu wavuni, huku juhudi za mabeki wa Prisons kutaka kuuokoa kushindikana.

Dakika ya 25, Okwi alikosa bao alipounganisha krosi safi kutoka kwa Clatous Chama, lakini shuti lake lilipaa juu la lango wa wapinzani wao.

Kipindi cha pili, Prisons walilisakama lango la Simba kupitia kwa Salum Kimenya, Lambart Subianka, Adam Adam na wengine, lakini juhudi zao ziliishia miguuni kwa mabeki wa wapinzani wao wakiongozwa na Erasto Nyoni na Mohamed Hussein 'Zimbwe Jnr', pamoja na mikono ya mlinda mlando, Aishi Manula.

Ili kulinda bao hilo walilolipata mapema, Kocha wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems, aliamua kumtoa Okwi na kumwingiza Jonas Mkude ili kuimarisha safu ya kiungo na baadaye alimtoa Haruna Niyonzima na nafasi yake kuchukuliwa na Hassan Dilunga wakati Nicolas Gyan akichukua nafasi ya Zana Coulibaly baada ya kuona mashambulizi ya Prisons dakika za mwisho yanapitia upande wake.

Kwa upande wa Prisons, imefungwa mechi mbili mfululizo, kwani Alhamisi ilikiona cha moto ilipochapwa mabao 2-1 dhidi ya Yanga kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, sasa inakamata nafasi ya tisa, ikisalia na pointi zake 42, ikicheza mechi 34 nayo pia ikiwa imebakisha mechi nne, ingawa haiko kwenye tishio la timu zilizo kwenye janga la kushuka daraja.

Simba itarejea jijini leo tayari kuwasubiri Coastal Union kutoka Tanga katika mchezo mwingine wa ligi hiyo utakaochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Uhuru wakati Azam FC leo watakuwa ugenini Shinyanga kuwavaa Stand United.

# Yanga, Lipuli FC hapatoshi Iringa leo

**Na Somoe Ng'itu**

VINARA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, wanatarajia kuwakabili Lipuli FC katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la FA itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM, Samora mjini Iringa.

Tayari Azam FC ya jijini hapa imeshatinga fainali ya michuano hiyo baada ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya KMC FC katika mchezo uliochezwa Ijumaa iliyopita kwenye Uwanja wa Azam Complex.

Yanga itashuka kwenye uwanja huo ikiwa na kumbukumbu ya kichapo cha bao 1-0 walichokipata kutoka kwa wenyeji wao katika mechi ya mzunguko wa pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mratibu wa Yanga, Hafidh Saleh, alisema kuwa wachezaji wao wako tayari kwa mchezo huo ambao wanaufananisha na fainali.

Saleh alisema kuwa watapambana ili kusaka ushindi kwa sababu wanahitaji kuendelea mbele na kuchukua kikombe cha michuano hiyo ambacho msimu uliopita kilichukuliwa na Mtibwa Sugar ya Morogoro.

"Tuko tayari kwa mapambano, tunajua mechi haitakuwa rahisi, lakini kwetu kila mechi ni sawa na fainali, tumejipanga kupambana mpaka dakika ya mwisho," Saleh alisema.

Kocha Mkuu wa Lipuli, Selemani Matola, aliliambia gazeti hili kuwa hiyo ni mechi muhimu zaidi kwao msimu huu kwa sababu wakishinda na kusonga mbele watakuwa wamekaribia kutimiza ndoto zao.

Matola alisema kuwa baada ya kupokea nafasi ya kutwaa ubingwa, sasa wanaamini michuano hiyo ndiyo imebakia kwa wao kupambana kupata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

"Tunajua mechi haitakuwa rahisi, Yanga ni timu nzuri na sisi pia ni wazuri, tunahitaji kuweka heshima na rekodi, tunajua tukishinda tutakaribia kucheza mashindano ya kimataifa ambayo kwa Wana-Iringa itakuwa ni mafanikio makubwa," alisema kocha huyo.

**WACHANGIWA MAMILIONI**

Wakati mchakato wa uchaguzi wa Yanga ukiendelea, jumla ya Sh. milioni 20 zilikusanywa kutoka kwa wanachama pamoja na "matajiri" wachache wa klabu hiyo ambao walihudhuria mkutano huo uliofanyika kwenye Ukumbi wa Bwalo la Polisi Oysterbay.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >